

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)



Ina Aya 35 **SURATUL AHQAF** *Ina Makara 4*

(Imeteremka Makka)

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

حٰمٓ ①

1. Haa Mym.

تَنْزِيْلُ الْكِتٰبِ مِنَ اللّٰهِ الْعَزِيْزِ الْحَكِيْمِ ②

2. Uteremsho wa Kitabu (hiki) umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, (na) Mwenye hikima.

مَا خَلَقْنَا السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَآ اِلَّا بِالْحَقِّ وَاَجَلٍ مُّسَمًّى ؕ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا عَمَّآ اُنْذِرُوْا مُعْرِضُوْنَ ③

3. Hatukuziumba mbingu na ardhi wala yaliyomo baina yake ila kwa haki na kwa muda uliowekwa; na wale wanaokufuru wanayapuuza (maonyo) wanayoonywa.

قُلْ اَرَءَيْتُمْ مَّا تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ اَرُوْنِيْ مَاذَا خَلَقُوْا مِنَ الْاَرْضِ اَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمٰوٰتِ ؕ اِيْتُوْنِيْ بِكِتٰبٍ مِّنْ قَبْلِ هٰذَآ اَوْ اَثٰرَةٍ مِّنْ عِلْمٍ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ④

4. Sema: "Je! Mnaonaje wale mnaowaabudu mkamwacha Mwenyezi Mungu?" Nionyesheni kipi walichokiumba katika ardhi, au wanayoshirika katika mbingu? Nileteeni Kitabu kilichokuwa kabla ya hiki au alama yoyote ya ilimu (ya kuthubutisha haya mnayoyasema); ikiwa mnasema kweli.

وَمَنْ اَضَلُّ مِمَّنْ يَّدْعُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَنْ لَّا يَسْتَجِيْبُ لَهٗٓ اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ وَهُمْ عَنْ دُعَآئِهِمْ غٰفِلُوْنَ ⑤

5. Na wapotofu (wapotevu) wakubwa ni nani kuliko wale wanaowaomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu ambao hawatawajibu mpaka siku ya Kiama, na hawatambui dua zao.

وَاِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوْا لَهُمْ اَعْدَآءً وَّكَانُوْا بِعِبَادَتِهِمْ كٰفِرِيْنَ ⑥

6. Na (ambao) watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيٰتُنَا بَيِّنٰتٍ قَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لِلْحَقِّ لَمَّا جَآءَهُمْ ۙ هٰذَا سِحْرٌ مُّبِيْنٌ ⑦

7. Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, wale waliokufuru husema juu ya haki inapowajia: "Huu ni uchawi ulio dhahiri."

اَمْ يَقُوْلُوْنَ افْتَرٰىهُ ؕ قُلْ اِنِ افْتَرَيْتُهٗ فَلَا تَمْلِكُوْنَ لِيْ مِنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا ؕ هُوَ اَعْلَمُ بِمَا

8. Au wanasema: "Ameyatunga, (ameyabuni ameyazua) mwenyewe." Sema: "Ikiwa nimeyatunga mimi, basi hamuwezi kunifaa chochote mbele ya

---

4. Makadiyani wamepachikia katika hii Aya waliyoifanya ya 5 maneno haya:— "Hao wanaosadiki ya kuwa Nabii Isa alipata kuumba vitu, sasa watokee kujibu hoja hii ya Mwenyezi Mungu . . . ." Wametia haya ili kupinga ile miujiza ya Nabii Isa aliyopewa na Mwenyezi Mungu. Na moja katika hiyo ni kufanya ndege wa udongo wakaruka, kisha wakaanguka wakafa. Sisi tunamsadiki Mwenyezi Mungu alivyosema kama tulivyobainisha haya katika marejezo ya Aya ya 49 ya Surat *Aali Imran*. Wao wanamkanusha Mwenyezi Mungu — khiyari yao.

5-6. Mara nyingi zimekuja simango huzi za kusimwangwa wanaowaomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu; Yeye ndiye ajuaye mnayoyashughulikia. Yeye anatosha kuwa Shahidi baina yangu na nyinyi; Naye ni Mwingi wa msamaha, Mwingi wa rehema."

تُفِيضُونَ فِيهِ ۚ كَفَىٰ بِهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۖ وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٨﴾

9. Sema: "Mimi si kiroja (mpya), katika Mitume. Wala sijui nitakavyofanywa mimi wala mtakavyofanywa nyinyi. Sifuati ila yaliyofunuliwa kwangu; na si kuwa miye lo lote ila ni Mwonyaji tu ninayedhihirisha (kila linalohitajia)."

قُلْ مَا كُنتُ بِدْعًا مِّنَ الرُّسُلِ وَمَا أَدْرِي مَا يُفْعَلُ بِي وَلَا بِكُمْ ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ وَمَا أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٩﴾

10. Sema: "Mnaonaje kikiwa (kitabu hiki) kimetoka kwa Mwenyezi Mungu; nanyi mumekikanusha, na mashahidi miongoni mwa wana wa Israili, (Mayahudi waliosilimu) walishuhudia juu ya mfano wa haya na wakaamini haya, na nyinyi mnafanya kiburi; (si hatari juu yenu?) Kwa yakini Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu."

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِن كَانَ مِنْ عِندِ اللَّهِ وَكَفَرْتُم بِهِ وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّن بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَىٰ مِثْلِهِ فَآمَنَ وَاسْتَكْبَرْتُمْ ۖ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠﴾

11. Na waliokufuru waliwaambia Waislamu: "Lau ingalikuwa (dini hii) ni ya Kheri wasingetutangulia (hao makafiri waliokufuata)." Na walipokosa kuongoka kwa haya basi wanasema: "Huu ni uwongo wa (watu wa) zamani."

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا لَوْ كَانَ خَيْرًا مَّا سَبَقُونَا إِلَيْهِ ۚ وَإِذْ لَمْ يَهْتَدُوا بِهِ فَسَيَقُولُونَ هَٰذَا إِفْكٌ قَدِيمٌ ﴿١١﴾

12. Na kabla yake kilikuwako Kitabu cha Musa, kiongozi na chenye rehema. Na hiki ni kitabu cha kusadikisha (vitabu vilivyotangulia vya Mwenyezi Mungu) na (kilichokuja) kwa lugha ya Kiarabu, ili kiwaonye wale waliodhulumu (nafsi zao) na kiwe bishara, (chenye habari za furaha) kwa watendao wema.

وَمِن قَبْلِهِ كِتَابُ مُوسَىٰ إِمَامًا وَرَحْمَةً ۚ وَهَٰذَا كِتَابٌ مُّصَدِّقٌ لِّسَانًا عَرَبِيًّا لِّيُنذِرَ الَّذِينَ ظَلَمُوا وَبُشْرَىٰ لِلْمُحْسِنِينَ ﴿١٢﴾

13. Hakika wale waliosema: "Mola wetu ni Mwenyezi Mungu," kisha wakatengenea, hawatakuwa na hofu (siku ya kufa kwao wala baadaye) wala hawatahuzunika.

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوا فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٣﴾

14. Hao ndio watu wa Peponi, watakaa humo (daima): ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda.

أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ خَالِدِينَ فِيهَا ۖ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

15. Na tumemuusia mwanaadamu afanye wema kwa wazazi wake. Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu na akamza kwa taabu. Na kubeba mimba yake hata kumwachisha ziwa; (uchache wake) ni mezi thalathini. Hata anapofikia baleghe

وَوَصَّيْنَا الْإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا ۖ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا ۖ وَحَمْلُهُ وَفِصَالُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا ۚ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَبَلَغَ أَرْبَعِينَ

9-13. Makadiyani katika hizi Aya walizozifanya ni ya 10 ya na 14 wametia, kisirisiri, ukafiri wao wa kumdaia Uume mtu wao. Tumeyajibu haya mara nyingi. Na mahala pa mwisho ni katika marejezo ya Aya ya 40 ya *Suratul Ahzab*.

15-15. Wanavyokuwa watoto wazuri na vipi watakavyolipwa.

سَنَةً ۚ قَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِيٓ أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ ٱلَّتِيٓ
أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَٰلِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَٰلِحًا
تَرْضَىٰهُ وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِيٓ ۖ إِنِّي تُبْتُ
إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ ٱلْمُسْلِمِينَ ﴿١٥﴾

yake na akawa mwenye umri wa miaka arubaini, (mtoto mwema) husema:— "Ee Mola wangu! Niwezeshe nishukuru neema zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na niwezeshe nifanye vitendo vizuri unavyovipenda, na unitengenezee watoto wangu; kwa yakini ninatubu kwako; na hakika mimi ni miongoni mwa waliosilimu (walionyenyekea)."

أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ نَتَقَبَّلُ عَنْهُمْ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا۟
وَنَتَجَاوَزُ عَن سَيِّـَٔاتِهِمْ فِيٓ أَصْحَٰبِ ٱلْجَنَّةِ ۖ
وَعْدَ ٱلصِّدْقِ ٱلَّذِي كَانُوا۟ يُوعَدُونَ ﴿١٦﴾

16. Hao ndio tunaowakubalia vitendo vyao vyema walivyovifanya, na tunayapita kando makosa yao, (tunayasamehe); (watakuwa) miongoni mwa watu wa Peponi: miadi ya kweli waliyoahidiwa.

وَٱلَّذِي قَالَ لِوَٰلِدَيْهِ أُفٍّ لَّكُمَآ أَتَعِدَانِنِيٓ أَنْ
أُخْرَجَ وَقَدْ خَلَتِ ٱلْقُرُونُ مِن قَبْلِي ۖ
وَهُمَا يَسْتَغِيثَانِ ٱللَّهَ وَيْلَكَ ءَامِنْ إِنَّ وَعْدَ ٱللَّهِ
حَقٌّ فَيَقُولُ مَا هَٰذَآ إِلَّآ أَسَٰطِيرُ ٱلْأَوَّلِينَ ﴿١٧﴾

17. Na ambaye anawaambia wazazi wake: "Kefule nyi! Oh! Mnanitishia kuwa nitafufuliwa; na hali karne nyingi, (watu wengi) zimekwisha pita kabla yangu (wala hazikufufuliwa)?" Na hao (wazee wake) wawili huomba msaada wa Mwenyezi Mungu; (na humwambia mtoto wao:) "Ole wako! Amini (haya unayoambiwa). Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli." Lakini yeye husema: "Hayakuwa haya (mnayoyasema) ila ni visa vya watu wa kale (tu si maneno ya kweli)."

أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ ٱلْقَوْلُ فِيٓ أُمَمٍ قَدْ خَلَتْ
مِن قَبْلِهِم مِّنَ ٱلْجِنِّ وَٱلْإِنسِ ۖ إِنَّهُمْ كَانُوا۟
خَٰسِرِينَ ﴿١٨﴾

18. Hao ndio ambao imelazimika hukumu juu yao (ya kutiwa Motoni), pamoja na mataifa yaliyopita kabla yao ya majini na watu, hakika hao ndio waliojitia khasarani.

وَلِكُلٍّ دَرَجَٰتٌ مِّمَّا عَمِلُوا۟ ۖ وَلِيُوَفِّيَهُمْ أَعْمَٰلَهُمْ
وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٩﴾

19. Na (viumbe) wote watakuwa na daraja (zao mbali mbali) kwa yale waliyoyatenda, na ili (Mungu) awalipe (malipo ya) vitendo vyao; nao hawatadhulumiwa.

وَيَوْمَ يُعْرَضُ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ عَلَى ٱلنَّارِ أَذْهَبْتُمْ
طَيِّبَٰتِكُمْ فِي حَيَاتِكُمُ ٱلدُّنْيَا وَٱسْتَمْتَعْتُم بِهَا ۖ
فَٱلْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ ٱلْهُونِ بِمَا كُنتُمْ
تَسْتَكْبِرُونَ فِي ٱلْأَرْضِ بِغَيْرِ ٱلْحَقِّ وَبِمَا كُنتُمْ
تَفْسُقُونَ ﴿٢٠﴾ ع ٢

20. Na (wakumbushe) siku watakapowekwa waliokufuru mbele ya Moto (waambiwe:) Mlipoteza vitu vyenu vizuri katika maisha yenu ya dunia (basi hamtavipata leo hapa). Nyinyi mlijifurahisha navyo (huko); basi leo mtapewa adhabu ya fedheha kwa sababu ya kule kujivuna kwenu bure duniani, na kwa sababu ya kule kuasi kwenu.

وَٱذْكُرْ أَخَا عَادٍ ۖ إِذْ أَنذَرَ قَوْمَهُۥ بِٱلْأَحْقَافِ
وَقَدْ خَلَتِ ٱلنُّذُرُ مِنۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِۦٓ

21. Na (wakumbushe) mwenziwao Kina Aad, (yaani Nabii Hudi); alipowaonya kaumu yake katika (nchi yenye) machuguu ya mchanga. Na kwa yakini Waonyaji wengi walitokea kabla yake na nyuma

17-18. Walivyo baadhi ya watoto wabaya na namna watakavyolipwa.

20. Watakavyojibiwa waliotupa Akhera kwa starehe za dunia za dhuluma na haramu.

21. Habari za watu wa Nabii Hudi; na tumebainisha kuwa walikuwa wakikaa kusini ya Bara Arabu na kuwa huko wakati huo kulikuwa mahala pa ustaarabu mkubwa.

أَلَّا تَعْبُدُوٓا۟ إِلَّا ٱللَّهَ ۖ إِنِّىٓ أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٢١﴾

yake; (akawaambia): "Msimuabudu yoyote ila Mwenyezi Mungu: hakika mimi nakuhofieni adhabu ya siku iliyo kuu."

قَالُوٓا۟ أَجِئْتَنَا لِتَأْفِكَنَا عَنْ ءَالِهَتِنَا ۖ فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ إِن كُنتَ مِنَ ٱلصَّٰدِقِينَ ﴿٢٢﴾

22. Wakasema: "Oh! Umetujia ili ututenge mbali na miungu yetu? Basi tuletee unayotuahidi, (kuwa utatuletea); ikiwa umo miongoni mwa wasemao kweli."

قَالَ إِنَّمَا ٱلْعِلْمُ عِندَ ٱللَّهِ ۖ وَأُبَلِّغُكُم مَّآ أُرْسِلْتُ بِهِۦ وَلَٰكِنِّىٓ أَرَىٰكُمْ قَوْمًا تَجْهَلُونَ ﴿٢٣﴾

23. Akasema: "Ilimu hasa iko kwa Mwenyezi Mungu tu, nami ninakufikishieni yale niliyotumwa kwayo, walakini ninakuoneni kuwa nyinyi ni watu mfanyao mambo ya ujinga."

فَلَمَّا رَأَوْهُ عَارِضًا مُّسْتَقْبِلَ أَوْدِيَتِهِمْ قَالُوا۟ هَٰذَا عَارِضٌ مُّمْطِرُنَا ۚ بَلْ هُوَ مَا ٱسْتَعْجَلْتُم بِهِۦ ۖ رِيحٌ فِيهَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢٤﴾

24. Basi walipoliona wingu likiyaelekea mabonde yao, walisema: "Wingu hili la kutunyeshea mvua." (Wakaambiwa) "Bali haya ni ile mliyokuwa mkitaka ije kwa upesi, (adhabu ya Mwenyezi Mungu). Ni upepo ambao ndani yake iko adhabu iumizayo."

تُدَمِّرُ كُلَّ شَىْءٍۭ بِأَمْرِ رَبِّهَا فَأَصْبَحُوا۟ لَا يُرَىٰٓ إِلَّا مَسَٰكِنُهُمْ ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْقَوْمَ ٱلْمُجْرِمِينَ ﴿٢٥﴾

25. "Unaoangamiza kila kitu kwa amri ya Mola wake." Basi wakawa si wenye kuonekana tena ila nyumba zao tu (ndizo zilizosalia). Hivyo ndivyo tuwalipavyo watu waovu.

وَلَقَدْ مَكَّنَّٰهُمْ فِيمَآ إِن مَّكَّنَّٰكُمْ فِيهِ وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَأَبْصَٰرًا وَأَفْـِٔدَةً فَمَآ أَغْنَىٰ عَنْهُمْ سَمْعُهُمْ وَلَآ أَبْصَٰرُهُمْ وَلَآ أَفْـِٔدَتُهُم مِّن شَىْءٍ إِذْ كَانُوا۟ يَجْحَدُونَ بِـَٔايَٰتِ ٱللَّهِ وَحَاقَ بِهِم مَّا كَانُوا۟ بِهِۦ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٢٦﴾

26. Na bila shaka tuliwastawisha katika yale tusiyokustawisheni nyinyi, na tuliwapa masikio na macho na nyoyo; lakini masikio yao na macho yao na nyoyo zao hazikuwafaa chochote walipokuwa wakikanusha Aya za Mwenyezi Mungu, na yakawazunguka yale waliyoyafanyia mzaha.

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا مَا حَوْلَكُم مِّنَ ٱلْقُرَىٰ وَصَرَّفْنَا ٱلْـَٔايَٰتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٧﴾

27. Na hakika tuliiangamiza miji iliyokuzungukeni, na tuliwabainishia Aya (zetu) ili warejee (lakini hawakurejea).

فَلَوْلَا نَصَرَهُمُ ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُوا۟ مِن دُونِ ٱللَّهِ قُرْبَانًا ءَالِهَةً ۖ بَلْ ضَلُّوا۟ عَنْهُمْ ۚ وَذَٰلِكَ إِفْكُهُمْ وَمَا كَانُوا۟ يَفْتَرُونَ ﴿٢٨﴾

28. Basi mbona haikuwasaidia miungu ile waliyoishika wakamuacha Mwenyezi Mungu ili iwakaribishe kwake? Bali imewapotea (hawakuiona); na huo ndio uwongo wao na waliyokuwa wakiutunga.

وَإِذْ صَرَفْنَآ إِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ ٱلْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ ٱلْقُرْءَانَ ۖ فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوٓا۟ أَنصِتُوا۟ ۖ فَلَمَّا قُضِىَ وَلَّوْا۟ إِلَىٰ قَوْمِهِم مُّنذِرِينَ ﴿٢٩﴾

29. Na (wakumbushe) tulipokuletea kundi la majini (kuja kwako) kusikiliza Qurani. Basi walipoihudhuria walisema (kuambiana):— "Nyamazeni (msikilizeni maneno ya Mwenyezi Mungu)." Na ilipokwisha (somwa) walirudi kwa jamaa zao wakiwaonya.

---

29. Mtume kama alivyopelekwa kwa wanadamu ndivyo alivyopelekwa kwa majini, kama Qurani nzima na Hadithi za Mtume zinavyoonyesha. Lakini namna ya alivyokuwa akikutana nao hatujui sisi. Tuna yakini tu kuwa akikutana nao na akiwafunza yaliyo juu yao. Na wakati mwengine wakitoa jawabu nzuri kuliko za binaadamu, kama pale waliposomewa *Suratur Rahman* katika zile "*Fabiayyi A-alaai Rabbikumaa Tukadhdhiban*" yaani "basi ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha?" Basi kila Mtume akifika kipande hiki walikuwa wakisema

قَالُوا يٰقَوْمَنَآ إِنَّا سَمِعْنَا كِتٰبًا أُنْزِلَ مِنْۢ بَعْدِ
مُوسٰى مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَهْدِىٓ إِلَى الْحَقِّ
وَإِلٰى طَرِيقٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٣٠﴾

30. Wakasema: "Enyi watu wetu! Hakika tumesikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake na kinachoongoa katika haki na katika njia iliyonyoka."

يٰقَوْمَنَآ أَجِيبُوا دَاعِىَ اللَّهِ وَءَامِنُوا بِهِۦ يَغْفِرْ لَكُم
مِّن ذُنُوبِكُمْ وَيُجِرْكُم مِّنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣١﴾

31. "Enyi watu wetu! Muitikieni Mlingani, (Muitaji) wa Mwenyezi Mungu na muaminini, atakusameheni (Mwenyezi Mungu) madhambi yenu na atakukingeni na adhabu iumizayo."

وَمَن لَّا يُجِبْ دَاعِىَ اللَّهِ فَلَيْسَ بِمُعْجِزٍ
فِى الْأَرْضِ وَلَيْسَ لَهُۥ مِن دُونِهِۦٓ أَوْلِيَآءُ
أُولٰٓئِكَ فِى ضَلٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٣٢﴾

32. "Na wasio muitikia Muitaji wa Mwenyezi Mungu, basi wao hawatamshinda (asiwapate) hapa katika ardhi, wala hawatakuwa na walinzi mbele yake. Hao wamo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri."

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِى خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضَ
وَلَمْ يَعْىَ بِخَلْقِهِنَّ بِقَٰدِرٍ عَلٰٓى أَن يُحْۦِىَ الْمَوْتٰى
بَلٰٓى إِنَّهُۥ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٣﴾

33. Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu — aliyeziumba mbingu na ardhi na hakuchoka kwa kuziumba — Ana uweza wa kuwafufua wafu? Naam, hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.

وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ أَلَيْسَ
هٰذَا بِالْحَقِّ قَالُوا بَلٰى وَرَبِّنَا قَالَ فَذُوقُوا
الْعَذَابَ بِمَا كُنتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٤﴾


34. Na (wakumbushe) siku watakayopelekwa makafiri Motoni (waambiwe): "Je! Haya si kweli? (Nikiini macho tu?)" Waseme: "Naam! Wallahi (ni kweli)" Aseme (Mwenyezi Mungu): "Basi onjeni adhabu kwa sababu ya kule kukufuru kwenu."

فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ أُولُوا الْعَزْمِ مِنَ الرُّسُلِ
وَلَا تَسْتَعْجِل لَّهُمْ كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَ مَا
يُوعَدُونَ لَمْ يَلْبَثُوٓا إِلَّا سَاعَةً مِّن نَّهَارٍ
بَلٰغٌ فَهَلْ يُهْلَكُ إِلَّا الْقَوْمُ الْفَٰسِقُونَ ﴿٣٥﴾

35. Basi subiri kama walivyosubiri wale Mitume wenye ustahimilivu mkubwa (kama Nabii Nuhu na Ibrahimu na Musa na Isa); wala usiwahimizie (adhabu). Siku watakayoyaona waliyoahidiwa itakuwa kama kwamba hawakukaa ulimwenguni ila saa moja ya mchana. (Haya mnayoambiwa) ndio ufikisho (ulio kamili); kwani huangamizwa (wengine) ila watu waovu tu?

"Laa Shay-a Min Niamika Rabbanaa Nukadhdhibu, Falakal Hamdu" yaani "Hakuna yoyote katika neema zako tunayoikadhibisha. Bali tunashukuru." Na Mtume alipowasomea binadamu hawakujibu chochote. Mtume akawatahayarisha akawambia "Ndugu zenu wa Kijini walijibu jawabu nzuri waliposikia haya." Hadithi hii wameitaja Maimamu hawa: Attirmidhy, Al Hakim, Ibnul Mundhir, Ibn Mardawayh, Al Bayhaqy na wengineo.

Katika Aya hii waliyoifanya ya 30 wamekanusha tena Majini. Habari hii tumekwisha kujibu katika marejezo ya Aya 112 ya *Suratul An-am* na kwingineko.



Ina Aya 38

SURAT MUHAMMAD
(Imeteremka Madina)

Ina Makaru 4

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

اَلَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ اَضَلَّ اَعْمَالَهُمْ ①

1. **Wale waliokufuru na wakajizuilia (na wakazuilia watu) njia ya Mwenyezi Mungu, Yeye atavithubutishia uovu vitendo vyao.**

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَاٰمَنُوْا بِمَا نُزِّلَ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّهُوَ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّهِمْ ۙ كَفَّرَ عَنْهُمْ سَيِّاٰتِهِمْ وَاَصْلَحَ بَالَهُمْ ②

2. **Na wale walioamini na wakatenda mema na wakaamini yaliyoteremshwa juu ya Muhammad — nayo ni haki iliyotoka kwa Mola wao — hawa atawafutia makosa yao na atastawisha hali yao.**

ذٰلِكَ بِاَنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوا اتَّبَعُوا الْبَاطِلَ وَاَنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّبَعُوا الْحَقَّ مِنْ رَّبِّهِمْ ۭ كَذٰلِكَ يَضْرِبُ اللّٰهُ لِلنَّاسِ اَمْثَالَهُمْ ③

3. **Hayo ni kwa sababu wale waliokufuru walifuata upotofu (upotevu), na wale walioamini wamefuata haki iliyotoka kwa Mola wao. Namna hivi Mwenyezi Mungu anavyowapigia, (anavyowaeleza) watu mifano yao.**

فَاِذَا لَقِيْتُمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَضَرْبَ الرِّقَابِ ۭ حَتّٰٓى اِذَآ اَثْخَنْتُمُوْهُمْ فَشُدُّوا الْوَثَاقَ ۙ فَاِمَّا مَنًّۢا بَعْدُ وَاِمَّا فِدَاۗءً حَتّٰى تَضَعَ الْحَرْبُ اَوْزَارَهَا ۚ ذٰلِكَ ۭ وَلَوْ يَشَاۗءُ اللّٰهُ لَانْتَصَرَ مِنْهُمْ ۙ وَلٰكِنْ لِّيَبْلُوَا بَعْضَكُمْ بِبَعْضٍ ۭ وَالَّذِيْنَ قُتِلُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ فَلَنْ يُّضِلَّ اَعْمَالَهُمْ ④

4. **Basi mnapokutana (vitani) na wale waliokufuru wapigeni katika shingo zao (wafe mara moja); mpaka mkiwashinda sana, hapo wafungeni (muwachukue makwenu, hali ya kuwa ni mateka); tena wawacheni kwa ihsani (wende zao makwao) au kwa kujikomboa. (Kila vikitokea vita fanyeni vivi hivi) hata vita vitue mizigo yake, (mpaka mambo ya vita yaondoke). Ndivyo hivyo. Na lau angalitaka Mwenyezi Mungu angejilipiza kisasi kwao, (makafiri Yeye mwenyewe); lakini (vita vimetokea) ili awatie mtihani baadhi yenu kwa wengine. Na wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu, hatavipuuza vitendo vyao.**

سَيَهْدِيْهِمْ وَيُصْلِحُ بَالَهُمْ ⑤

5. **Atawaongoa na kustawisha hali yao.**

وَيُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ ⑥

6. **Na atawaingiza katika Pepo aliyowajulisha.**

---

4. Waislamu ikiwapasa kupigana na makafiri wakapatikana mateka basi mkubwa wa Waislamu ana haki ya kuwafanyia moja katika matano haya: Ima (a) Awaue. (lakini wale wanaume tu wenye khatari juu ya Uislamu); au (b) Awafanye watumwa, walio wanaume na wanawake pia; au (c) Awatoze wote kikomboleo cha mali; au (d) Wabadilishwe kwa mateka wa Kiislamu waliotekwa na makafiri; au (e) Wawachiwe bure wende zao.
Na hizi hukumu hatu za mwisho ndizo zilizotajwa hapa katika Qurani.

7. Enyi mlioamini! Mkiinusuru dini ya Mwenyezi Mungu, naye atakunusuruni na ataithubutisha miguu yenu.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنْ تَنْصُرُوا اللّٰهَ يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ اَقْدَامَكُمْ ۝٧

8. Na wale waliokufuru, basi kwao ni maangamizo na atavipuuza vitendo vyao.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَتَعْسًا لَّهُمْ وَاَضَلَّ اَعْمَالَهُمْ ۝٨

9. Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha, (ataviondoshea thawabu) vitendo vyao.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ كَرِهُوْا مَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فَاَحْبَطَ اَعْمَالَهُمْ ۝٩

10. Je! Hawakutembea katika ardhi wakaona umekuwaje mwisho wa wale waliowatangulia? Mwenyezi Mungu aliwaangamiza; na kwa makafiri (hawa) itakuwa (adhabu) kama hiyo.

اَفَلَمْ يَسِيْرُوْا فِى الْاَرْضِ فَيَنْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۭ دَمَّرَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ ۭ وَلِلْكٰفِرِيْنَ اَمْثَالُهَا ۝١٠

11. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini, (anawapenda); lakini makafiri hawana mlinzi wao.

ذٰلِكَ بِاَنَّ اللّٰهَ مَوْلَى الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَاَنَّ الْكٰفِرِيْنَ لَا مَوْلٰى لَهُمْ ۝١١ ع

12. Kwa hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walioamini na wakafanya mema, (atawaingiza) katika mabustani yapitayo mito mbele yake. Lakini waliokufuru hujifurahisha (hapa duniani) na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makazi yao.

اِنَّ اللّٰهَ يُدْخِلُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ۭ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا يَتَمَتَّعُوْنَ وَيَاْكُلُوْنَ كَمَا تَاْكُلُ الْاَنْعَامُ وَالنَّارُ مَثْوًى لَّهُمْ ۝١٢

13. Na (watu wa) miji mingapi iliyokuwa yenye nguvu zaidi kuliko (watu wa) mji wako uliokutoa: Tuliwaangamiza wala hawakuwa na msaidizi.

وَكَاَيِّنْ مِّنْ قَرْيَةٍ هِىَ اَشَدُّ قُوَّةً مِّنْ قَرْيَتِكَ الَّتِيْٓ اَخْرَجَتْكَ ۚ اَهْلَكْنٰهُمْ فَلَا نَاصِرَ لَهُمْ ۝١٣

14. Je! Watu wenye kuwa na dalili zitokazo kwa Mola wao watakuwa sawa na watu waliopambiwa ubaya wa vitendo vyao (vibaya) na wakafuata matamanio ya nafsi zao?

اَفَمَنْ كَانَ عَلٰي بَيِّنَةٍ مِّنْ رَّبِّهٖ كَمَنْ زُيِّنَ لَهٗ سُوْۗءُ عَمَلِهٖ وَاتَّبَعُوْٓا اَهْوَاۗءَهُمْ ۝١٤

15. Mfano wa Pepo waliyoahidiwa watawa (wacha Mungu itakuwa hivi): imo mito ya maji yasiyovunda, na mito ya maziwa isiyoharibika ladha yake, na mito ya ulevi wenye ladha kwa wanywao, na mito ya asali iliyosafishwa; tena humo watapata matunda ya kila namna, na samahani kutoka kwa Mola wao. Basi hao watakuwa sawa na wale watakaokaa Motoni na kunyweshwa maji yachemkayo yatakayokata chango zao?

مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِيْ وُعِدَ الْمُتَّقُوْنَ ۭ فِيْهَآ اَنْهٰرٌ مِّنْ مَّاۗءٍ غَيْرِ اٰسِنٍ ۚ وَاَنْهٰرٌ مِّنْ لَّبَنٍ لَّمْ يَتَغَيَّرْ طَعْمُهٗ ۚ وَاَنْهٰرٌ مِّنْ خَمْرٍ لَّذَّةٍ لِّلشّٰرِبِيْنَ ۚ وَاَنْهٰرٌ مِّنْ عَسَلٍ مُّصَفًّى ۭ وَلَهُمْ فِيْهَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرٰتِ وَمَغْفِرَةٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ ۭ كَمَنْ هُوَ خَالِدٌ فِي النَّارِ وَسُقُوْا مَاۗءً حَمِيْمًا فَقَطَّعَ اَمْعَاۗءَهُمْ ۝١٥

16. Na wako miongoni mwao (hao makafiri) wanaokusikiliza; (nao hawasikii lolote kwani hawana nia khasa ya kusikiliza); hata wanapoondoka kwako

12. Tusiwe na sifa hii ya kikafiri ya kula na kustarehe tu basi.
16. Inataka unapoyasikia maneno ya haki uyasikilize vizuri uyatie akilini.

wanawauliza wale waliopewa ilimu (wakawaambia: "Vile Mtume) amesema nini sasa hivi?" Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewapiga muhuri nyoyoni mwao (amezifumba) na wakafuata matamanio ya nafsi zao.

عِنْدِكَ قَالُوْا لِلَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ مَاذَا قَالَ
انِفًا ؕ اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ طَبَعَ اللّٰهُ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ
وَاتَّبَعُوْٓا اَهْوَآءَهُمْ ﴿١٦﴾

17. Na wale wanaokubali kuongoka anawazidishia uongofu na anawapa (jaza) ya ucha Mungu wao.

وَالَّذِيْنَ اهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَّاٰتٰىهُمْ تَقْوٰىهُمْ ﴿١٧﴾

18. Kwani wanangoja jingine ila Kiama kiwajie kwa ghafula? Basi alama zake (hicho Kiama) zimekwisha kuja. Kutawafaa wapi kukumbuka wakati kitakapowajia?

فَهَلْ يَنْظُرُوْنَ اِلَّا السَّاعَةَ اَنْ تَاْتِيَهُمْ بَغْتَةً ۚ
فَقَدْ جَآءَ اَشْرَاطُهَا ۚ فَاَنّٰى لَهُمْ اِذَا جَآءَتْهُمْ
ذِكْرٰىهُمْ ﴿١٨﴾

19. Jua ya kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki ila Mwenyezi Mungu, na omba maghufira kwa dhambi zako na (dhambi) za Waislamu wanaume na Waislamu wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi na mahali penu pa kukaa.

فَاعْلَمْ اَنَّهٗ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنْۢبِكَ
وَلِلْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ
مُتَقَلَّبَكُمْ وَمَثْوٰىكُمْ ﴿١٩﴾ ع

20. Na walioamini, (kwa ajili ya zile balaa zinazowafika kwa makafiri) husema: "Kwa nini haiteremshwi Sura (ya kutupa ruhusa kupigana na makafiri wanaotupiga bure)?" Lakini inapoteremshwa Sura thabiti, na ndani yake ikatajwa habari ya vita, utawaona wale wenye maradhi katika nyoyo zao wanakutazama mtazamo wa anayezimia kwa mauti (kwa kuichukia hiyo amri ya kutoa ruhusa ya kupigana na makafiri). Basi ole wao! (Adhabu ya Mwenyezi Mungu imekwishawafika).

وَيَقُوْلُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَوْلَا نُزِّلَتْ سُوْرَةٌ ۚ فَاِذَآ
اُنْزِلَتْ سُوْرَةٌ مُّحْكَمَةٌ وَّذُكِرَ فِيْهَا الْقِتَالُ ۙ
رَاَيْتَ الَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ يَّنْظُرُوْنَ اِلَيْكَ
نَظَرَ الْمَغْشِيِّ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ؕ فَاَوْلٰى لَهُمْ ﴿٢٠﴾

21. (Yanayotakiwa ni) utii na kauli njema, (na wao hawana hata moja katika haya). Na jambo linapokwishaazimiwa (nawalifanye). Wakiwa wakweli kwa Mwenyezi Mungu bila shaka itakuwa bora kwao.

طَاعَةٌ وَّقَوْلٌ مَّعْرُوْفٌ ؕ فَاِذَا عَزَمَ الْاَمْرُ ۫ فَلَوْ
صَدَقُوا اللّٰهَ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ ﴿٢١﴾

22. Ndiyo yanayotarajiwa kwenu kufisidi katika ardhi na kuwakata jamaa zenu wakati mkipata ukubwa?

فَهَلْ عَسَيْتُمْ اِنْ تَوَلَّيْتُمْ اَنْ تُفْسِدُوْا فِي الْاَرْضِ
وَتُقَطِّعُوْٓا اَرْحَامَكُمْ ﴿٢٢﴾

---

17. Haya ndiyo hayo yanayosemwa kila siku kuwa wanaokubali kuongoka ndio anaowaongoa Mwenyezi Mungu.

19. Waislamu washughulikiane. Wawapendelee wenzi wao wanayojipendelea wenyewe nafsi zao. Basi hata dua wanazojiombea wawaombee na wenzi wao.

22. Inataka kijana akisha kupata isiwe kwake kuliza Mbwata, (kupiga makofi makalioni kwake) kuonyesha hana haja na watu wake. Sharti awashughulikie watu wake wa kiume na wa kike, kwa kiasi cha uweza wake, au Moto utakuwa maskani yake. Inataka kwa kila Muislamu awajue watu wake wote; apate kuwashughulikia kwa hali yake na mali yake kama ana uweza wa yote, au kwa hali tu ikiwa hana uweza wa mali. Mtume alikuwa akihimiza sana kila mtu kujijua namna alivyozalika, kwa upande wa kuumeni na wa kuukeni, na kujua namna alivyokhusika nao na kunasibika. Na kuwajua kila ambao kwa ajili yake walitaabika, ili awalipe ihsani zao zilizopita. Kulipa ihsani ni wajibu mkubwa kabisa. Na sisi tunapuuza.

23. Hao ndio Mwenyezi Mungu aliowalani akawatia uziwi na kuyapofoa macho yao.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فَأَصَمَّهُمْ وَأَعْمَىٰ أَبْصَارَهُمْ ﴿٢٣﴾

24. Je! Hawaizingatii hii Qurani? Au katika nyoyo zao kuna kufuli?

أَفَلَا يَتَدَبَّرُونَ الْقُرْآنَ أَمْ عَلَىٰ قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا ﴿٢٤﴾

25. Kwa hakika wale wanaorudi kimgongomgongo (kinyumenyume katika dini yao ya ukafiri baada ya kwisha kusilimu) baada ya kuwabainikia uwongofu, Shetani amewadanganya; na (Mwenyezi Mungu) anawapa muda.

إِنَّ الَّذِينَ ارْتَدُّوا عَلَىٰ أَدْبَارِهِم مِّن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْهُدَى ۙ الشَّيْطَانُ سَوَّلَ لَهُمْ وَأَمْلَىٰ لَهُمْ ﴿٢٥﴾

26. Huko (kuhisabika kuwa wamewacha dini) ni kwa sababu wao waliwaambia wale (makafiri) waliochukia yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu: "Tutakutiini katika baadhi ya mambo (yenu mnayokwenda kinyume na Muhammad)." Na Mwenyezi Mungu anajua siri zao.

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لِلَّذِينَ كَرِهُوا مَا نَزَّلَ اللَّهُ سَنُطِيعُكُمْ فِي بَعْضِ الْأَمْرِ ۖ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِسْرَارَهُمْ ﴿٢٦﴾

27. Basi itakuwaje (hali yao), Malaika watakapowafisha wakawa wanawapiga nyuso zao na migongo yao.

فَكَيْفَ إِذَا تَوَفَّتْهُمُ الْمَلَائِكَةُ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَارَهُمْ ﴿٢٧﴾

28. Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyomchukiza Mwenyezi Mungu na wakachukia yanayomridhisha, basi akaviondoshea thawabu vitendo vyao.

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمُ اتَّبَعُوا مَا أَسْخَطَ اللَّهَ وَكَرِهُوا رِضْوَانَهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ ﴿٢٨﴾

29. Je! Wale wenye maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hataidhihirisha bughudha yao?

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ أَن لَّن يُخْرِجَ اللَّهُ أَضْغَانَهُمْ ﴿٢٩﴾

30. Na kama tungependa tungekuonyesha (watu hao wenye bughudha na Uislamu) na ungewatambua kwa alama zao; lakini utaweza kuwafahamu kwa namna ya msemo (wao). Na Mwenyezi Mungu anavijua vitendo vyenu (vyote).

وَلَوْ نَشَاءُ لَأَرَيْنَاكَهُمْ فَلَعَرَفْتَهُم بِسِيمَاهُمْ ۚ وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ ۚ وَاللَّهُ يَعْلَمُ أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٠﴾

31. Na tutakufanyieni mitihani mpaka tuwadhihirishe (wajulikane) wale wanaopigania dini miongoni mwenu na wanaosubiri; nasi Tutadhihirisha habari zenu.

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ الْمُجَاهِدِينَ مِنكُمْ وَالصَّابِرِينَ ۖ وَنَبْلُوَ أَخْبَارَكُمْ ﴿٣١﴾

32. Kwa hakika wale waliokufuru na wakawazuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu na wakapinzana na Mtume, baada ya kuwabainikia uwongofu; wao hawamdhuru Mwenyezi Mungu chochote, na ataviangusha, (ataviondoshea thawabu) vitendo vyao.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَشَاقُّوا الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْهُدَىٰ لَن يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا ۗ وَسَيُحْبِطُ أَعْمَالَهُمْ ﴿٣٢﴾

33. Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٣﴾

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ مَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ ﴿٣٤﴾

34. Hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakafa, nao ni makafiri, Mwenyezi Mungu hatawasamehe (makosa yao).

فَلَا تَهِنُوا وَتَدْعُوا إِلَى السَّلْمِ وَأَنْتُمُ الْأَعْلَوْنَ وَاللَّهُ مَعَكُمْ وَلَنْ يَتِرَكُمْ أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٥﴾

35. Basi msiregee na kutaka suluhu; (piganeni nao maadui zenu), maana nyinyi ndio mtakaoshinda; na Mwenyezi Mungu Yu pamoja nanyi; wala hatakunyimeni (thawabu za) vitendo vyenu.

إِنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَلَهْوٌ وَإِنْ تُؤْمِنُوا وَتَتَّقُوا يُؤْتِكُمْ أُجُورَكُمْ وَلَا يَسْأَلْكُمْ أَمْوَالَكُمْ ﴿٣٦﴾

36. Hakika maisha ya dunia ni mchezo na upuuzi. Na kama mkiamini na kujilinda na mabaya, atakupeni (Mwenyezi Mungu) ujira wenu, wala hatakutakeni (mtoe kitu kikubwa katika) mali zenu.

إِنْ يَسْأَلْكُمُوهَا فَيُحْفِكُمْ تَبْخَلُوا وَيُخْرِجْ أَضْغَانَكُمْ ﴿٣٧﴾

37. Na kama akikutakeni hayo na kukushikilieni mtafanya ubahili; na atatoa mifundo yenu, (atadhihirisha bughudha yenu).

هَا أَنْتُمْ هَؤُلَاءِ تُدْعَوْنَ لِتُنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَمِنْكُمْ مَنْ يَبْخَلُ وَمَنْ يَبْخَلْ فَإِنَّمَا يَبْخَلُ عَنْ نَفْسِهِ وَاللَّهُ الْغَنِيُّ وَأَنْتُمُ الْفُقَرَاءُ وَإِنْ تَتَوَلَّوْا يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَالَكُمْ ﴿٣٨﴾ ع

38. Lo! Nyinyi mnaitwa mtoe (mali) katika njia ya Mwenyezi Mungu, na kuna wengine katika nyiye wanafanya ubakhili! Basi afanyaye ubakhili anaufanya ubakhili huo kwa (kuidhuru) nafsi yake mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, na nyinyi ndio makafiri. Na kama mkirudi nyuma (mkaupa mgongo Uislamu, Mwenyezi Mungu) ataleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi. (Watakuwa bora).

---

35. Muislamu asiwe dhalili wala asiwe mwenye kiburi, lakini awe mwenye kuchunga yake itibari. Udhalilifu sio Uislamu wala Ujeuri. Uislamu utunze haki yako na haki za wenzako.

36-37. Kila amali njema anazofanya mtu atalipwa, hata ndogo kabisa hii hata ya kiasi cha chembe ya khardali, kama alivyosema katika Aya ya 16 ya *Surat Luqman* na Aya ya 47 ya *Suratul Anbiyaa*.

38. Watu wakikataa kufanya mema siyo yatadoda mema, yasifanyike tena. La. Bali Mwenyezi Mungu atawawafikia watu wengine wafanye mema hayo watengenekewe hapa duniani na Akhera; na waharibikiwe hao waliokataa kuyafanya kote kuwili.

سُورَةُ الْفَتْحِ مَدَنِيَّةٌ (١١١) (٤٨) اٰيَاتُهَا ٢٩ رُكُوعَاتُهَا ٤

Ina Aya 29 *Ina Makuru 4*

SURATUL FAT-H
(Imeteremka Madina)

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ①

1. Bila shaka tumekwishakupa kushinda kuliko dhahiri

لِّيَغْفِرَ لَكَ اللّٰهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنۢبِكَ وَمَا تَاَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهٗ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطًا مُّسْتَقِيْمًا ②

2. Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yanayokuja, na kukutimizia neema zake na kukuongoa katika njia iliyonyoka

وَّيَنْصُرَكَ اللّٰهُ نَصْرًا عَزِيْزًا ③

3. Na akunusuru Mwenyezi Mungu nusura yenye nguvu kabisa.

هُوَ الَّذِيْٓ اَنْزَلَ السَّكِيْنَةَ فِيْ قُلُوْبِ الْمُؤْمِنِيْنَ لِيَزْدَادُوْٓا اِيْمَانًا مَّعَ اِيْمَانِهِمْ ۗ وَلِلّٰهِ جُنُوْدُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۭ وَكَانَ اللّٰهُ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ④

4. Yeye ndiye aliyeteremsha utulivu katika nyoyo za Waislamu ili waongezeke imani juu ya imani yao. Na majeshi ya mbingu na ardhi ni ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi (wa kila jambo) na Mwenye hikima

---

1. Mtume katika mwaka wa 6 alitoka na baadhi ya Masahaba zake kwenda Makka kwa ajili ya Hija ndogo, (*Al Umra*). Lakini alipokaribia Makka kwa meli kidogo tu hivi, Maqureshi walivinjari barabara wakamkatalia katakata kuingia Makka kufanya hiyo Ibada aliyoikusudia. Baada ya mashauriano mengi — na hata kukaribia kupigana — walifanyiana suluhu kuwa:

(a) Wasipigane sasa hivi;

(b) Mwakani mwezi kama huo waje kufanya Ibada hiyo, wala Maqureshi hawatawazuilia;

(c) Wasipigane tena muda wa miaka kumi — wawe wanaendeana watakavyo. Makafiri wa Makka wende Madina wakitaka, bila ya kudhuriwa. Na Waislamu wende Makka wakitaka — bila ya kutaabishwa.

(d) Na Waarabu wengine wakawa na haki ya kuingia katika mkataba huu — wasipigane na Mtume, na Mtume asipigane nao.

Basi ndiyo Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume kuwa Mwenyezi Mungu amempa kushinda kukubwa kwa kupatikana mkataba huu. Navyo ndivyo ilivyokuwa. Haikupita myaka miwili hivi ila Makka ilisilimu, na Bara Arabu yote nzima takriba.

Basi Sura hii ni katika Sura zilizompa Mtume moyo mkubwa kabisa zilipoteremka.

Hata baada ya myaka miwili hivi — Mtume alipokuwa anaingia Makka kisha kuiteka — aliingia na huku anaisoma hii *Suratul Fat-h* kwa matao yaliyotimia, na Sauti ya kupendeza kabisa. Mtume kama alivyokuwa na maneno mazuri MNO KABISA, na vitendo vizuri MNO KABISA, na sura nzuri MNO KABISA, basi vile vile alikuwa na sauti nzuri MNO KABISA. Kila chake kilikuwa kizuri mno kabisa. Na kila Mtume katika zama zake alikuwa namna hivi juu ya watu wote wa zama hizo. Basi wakahimizwa wa kila uma wawe kama wao: katika kuwa na vitendo vizuri kabisa na maneno mazuri mno kabisa, ila sura na sauti ndiyo hatuwezi kuzigeuza. Ama hayo ya vitendo na maneno tunao uweza. Basi haya natufanye kwa dhati haya tunayoyaweza, na tujitahidi japo kidogo kuigiza hata hayo tusiyoyaweza. Anayechokoachokoa — hata pasipochokoleka — hakosi kupata kitu.

4. Waislamu walitaka kula mori waukatae mkataba ule — kwani ulikuwa na shuruti nyingine ambazo dhahiri yake si nzuri juu ya Waislamu. Lakini Mwenyezi Mungu aliwapoza wakaukubali; ikapatikana hiyo fursa kubwa kabisa iliyopatikana. Hwenda ukakiona kitu kibaya, tahamaki kizuri kimekuwa, na chenye heba na muruwa.

لِّيُدْخِلَ الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ
مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا وَيُكَفِّرَ عَنْهُمْ
سَيِّاٰتِهِمْ ۚ وَكَانَ ذٰلِكَ عِنْدَ اللّٰهِ فَوْزًا عَظِيْمًا ۝٥

5. (Ameyafanya haya) ili awaingize Waislamu wanaume na Waislamu wanawake katika Mabustani yapitayo mito mbele yake, wakadumu huko milele, na awafutie makosa yao. Na huku ndiko kufaulu kukubwa mbele ya Mwenyezi Mungu

وَّيُعَذِّبَ الْمُنٰفِقِيْنَ وَالْمُنٰفِقٰتِ وَالْمُشْرِكِيْنَ
وَالْمُشْرِكٰتِ الظَّآنِّيْنَ بِاللّٰهِ ظَنَّ السَّوْءِ ۚ عَلَيْهِمْ
دَآئِرَةُ السَّوْءِ ۚ وَغَضِبَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ وَلَعَنَهُمْ
وَاَعَدَّ لَهُمْ جَهَنَّمَ ۚ وَسَآءَتْ مَصِيْرًا ۝٦

6. Na awaadhibu wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na washirikina wanaume na washirikina wanawake, wanaomdhania Mwenyezi Mungu dhana mbaya. Utawafikia mgeuko mbaya. Na Mwenyezi Mungu awakasirikie na kuwalani na kuwaandalia Jahanamu; nayo ni marejeo mabaya kabisa.

وَلِلّٰهِ جُنُوْدُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ وَكَانَ
اللّٰهُ عَزِيْزًا حَكِيْمًا ۝٧

7. Na majeshi ya mbingu na ardhi ni ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

اِنَّآ اَرْسَلْنٰكَ شَاهِدًا وَّمُبَشِّرًا وَّنَذِيْرًا ۝٨

8. Hakika tumekuleta uwe Shahidi na Mtoaji wa habari njema na Muonyaji

لِّتُؤْمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَتُعَزِّرُوْهُ وَتُوَقِّرُوْهُ ۚ
وَتُسَبِّحُوْهُ بُكْرَةً وَّاَصِيْلًا ۝٩

9. Ili Mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mumtukuze na mumuhishimu, na kumuadhimisha (Mwenyezi Mungu) asubuhi na jioni.

اِنَّ الَّذِيْنَ يُبَايِعُوْنَكَ اِنَّمَا يُبَايِعُوْنَ اللّٰهَ ۚ
يَدُ اللّٰهِ فَوْقَ اَيْدِيْهِمْ ۚ فَمَنْ نَّكَثَ
فَاِنَّمَا يَنْكُثُ عَلٰى نَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ اَوْفٰى بِمَا عٰهَدَ
عَلَيْهُ اللّٰهَ فَسَيُؤْتِيْهِ اَجْرًا عَظِيْمًا ۝١٠ ع

10. Bila shaka wale wanaofungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi (hizi) anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na atekelezaye aliyomuahidi Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) atamlipa ujira mkubwa.

سَيَقُوْلُ لَكَ الْمُخَلَّفُوْنَ مِنَ الْاَعْرَابِ شَغَلَتْنَآ
اَمْوَالُنَا وَاَهْلُوْنَا فَاسْتَغْفِرْ لَنَا ۚ يَقُوْلُوْنَ
بِاَلْسِنَتِهِمْ مَّا لَيْسَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ ۚ قُلْ فَمَنْ
يَّمْلِكُ لَكُمْ مِّنَ اللّٰهِ شَيْئًا اِنْ اَرَادَ بِكُمْ
ضَرًّا اَوْ اَرَادَ بِكُمْ نَفْعًا ۚ بَلْ كَانَ اللّٰهُ بِمَا
تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرًا ۝١١

11. Watakwambia wale Mabedui waliokaa nyuma (wasende vitani wala hawana udhuru wowote; watajidai kutoa udhuru waseme): "Mali zetu na watu wetu walitushughulisha, basi tuombee msamaha." Wanasema kwa ndimi zao (maneno) yasiyokuwamo nyoyoni mwao. Sema: "Ni nani awezaye kukusaidieni chochote kwa Mwenyezi Mungu ikiwa anataka kukudhuruni au anataka kukunufaisheni?" Bali Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote.

---

10. Mtume — kama tunavyojua — ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Basi Mwenye kumpa ahadi Mtume ndiyo kama amempa ahadi Mwenyezi Mungu. Na *Alhamdu Lilahi;* walitekeleza ahadi yao waliyompa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu akafurahi nao, kama ilivyo katika Aya ya 18 ya Sura hii hii. Ahadi yenyewe ilikuwa kuwa: Ikibidi kupigana na Maqureshi watapigana tu — KUFA au KUPONA — hapana kukimbia.

11. Hawa ni wale wanafiki wanaotoa ahadi za uwongo kila siku ili wasende vitani:

Kama Islamu
Mponde mpondwe
Si hoja jamaa
Nendeni vitani
Kwenye maidani
Za Misikitini.

بَلْ ظَنَنْتُمْ اَنْ لَّنْ يَّنْقَلِبَ الرَّسُوْلُ وَالْمُؤْمِنُوْنَ
اِلٰٓى اَهْلِيْهِمْ اَبَدًا وَّزُيِّنَ ذٰلِكَ فِيْ قُلُوْبِكُمْ
وَظَنَنْتُمْ ظَنَّ السَّوْءِ ۖ وَكُنْتُمْ قَوْمًا بُوْرًا ⑫

12. Lakini mlidhani ya kwamba Mtume na Waislamu hawatarudi kabisa kwa watu wao, (watauawa vitani), na mkapambiwa hayo katika nyoyo zenu; na mlidhani dhana mbaya, na mumekuwa watu wanaoangamia.

وَمَنْ لَّمْ يُؤْمِنْ بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ فَاِنَّآ اَعْتَدْنَا
لِلْكٰفِرِيْنَ سَعِيْرًا ⑬

13. Na wasiomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi kwa hakika tumewaandalia makafiri hao Moto mkali.

وَلِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۭ يَغْفِرُ لِمَنْ يَّشَاۗءُ
وَيُعَذِّبُ مَنْ يَّشَاۗءُ ۭ وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ⑭

14. Na ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu, Humsamehe amtakaye (kwa kuwa amerejea kwake) na Humuadhibu amtakaye (kwa kuwa hakurejea kwake), na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

سَيَقُوْلُ الْمُخَلَّفُوْنَ اِذَا انْطَلَقْتُمْ اِلٰى مَغَانِمَ
لِتَاْخُذُوْهَا ذَرُوْنَا نَتَّبِعْكُمْ ۚ يُرِيْدُوْنَ
اَنْ يُّبَدِّلُوْا كَلٰمَ اللّٰهِ ۭ قُلْ لَّنْ تَتَّبِعُوْنَا كَذٰلِكُمْ
قَالَ اللّٰهُ مِنْ قَبْلُ ۚ فَسَيَقُوْلُوْنَ بَلْ
تَحْسُدُوْنَنَا ۭ بَلْ كَانُوْا لَا يَفْقَهُوْنَ اِلَّا قَلِيْلًا ⑮

15. Wale wakaao nyuma — mtakapokwenda kuchukua ngawira (nyara) — watasema: "Tuacheni tufuatane nanyi." Wanataka kuyabadili maneno ya Mwenyezi Mungu. Sema: "Hamtatufuata kabisa, Mwenyezi Mungu amekwishasema hivi zamani!" Hapo watasema: "Bali nyinyi mnatuhusudu (mnatuonea maya)." Siyo, bali walikuwa hawafahamu ila kidogo!

قُلْ لِّلْمُخَلَّفِيْنَ مِنَ الْاَعْرَابِ سَتُدْعَوْنَ اِلٰى
قَوْمٍ اُولِيْ بَاْسٍ شَدِيْدٍ تُقَاتِلُوْنَهُمْ اَوْ يُسْلِمُوْنَ ۚ
فَاِنْ تُطِيْعُوْا يُؤْتِكُمُ اللّٰهُ اَجْرًا حَسَنًا ۚ وَاِنْ
تَتَوَلَّوْا كَمَا تَوَلَّيْتُمْ مِّنْ قَبْلُ يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا
اَلِيْمًا ⑯

16. Waambie wale walioachwa nyuma katika watu wa majangwani: "Karibuni hivi mtaitwa kwenda kupigana na watu wenye mapigano makali, mtapigana nao au watasilimu; basi kama mkitii, (Mwenyezi Mungu) Atakupeni ujira mzuri; na mkigeuka kama mlivyogeuka kwanza, atakuadhibuni adhabu iumizayo."

لَيْسَ عَلَى الْاَعْمٰى حَرَجٌ وَّلَا عَلَى الْاَعْرَجِ حَرَجٌ
وَّلَا عَلَى الْمَرِيْضِ حَرَجٌ ۭ وَمَنْ يُّطِعِ اللّٰهَ
وَرَسُوْلَهٗ يُدْخِلْهُ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا
الْاَنْهٰرُ ۚ وَمَنْ يَّتَوَلَّ يُعَذِّبْهُ عَذَابًا اَلِيْمًا ⑰

17. Kipofu hana lawama, wala kiguru hana lawama, wala mgonjwa hana lawama (wasipokwenda vitani). Na anayemtii Mungu na Mtume wake atamwingiza mabustani yapitayo mito mbele yake. Na atakayegeuka upande, atamuadhibu adhabu iumizayo.

لَقَدْ رَضِيَ اللّٰهُ عَنِ الْمُؤْمِنِيْنَ اِذْ يُبَايِعُوْنَكَ
تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِيْ قُلُوْبِهِمْ فَاَنْزَلَ
السَّكِيْنَةَ عَلَيْهِمْ وَاَثَابَهُمْ فَتْحًا قَرِيْبًا ⑱

18. Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waislamu walipofungamana nawe chini ya mti; na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawapa kushinda kwa zama za karibu

---

15. Hapa wanalipwa hao wanafiki. Anaambiwa Mtume kuwa vita vya sasa hivi vyepesi, asiwachukue maadamu walikuwa wakivikimbia vile vigumu. Wawachwe waliokula uchungu wale utamu sasa; sio wale waliokuwa hawataki — pale zamani — kwenda vitani. Hawatataabika watu wengine wastarehe wengine. Aliyechuma juani ndiye ale kivulini; ila waliokuwa na udhuru — wakati huo — ndio wanaotolewa katika hukumu kali hii, kama ilivyo katika Aya ya 17 hapa chini.

18-21. Jaza ya hao Waislamu waliotoa ahadi kweli kweli.

وَّمَغَانِمَ كَثِيْرَةً يَّاْخُذُوْنَهَا ۗ وَكَانَ اللّٰهُ عَزِيْزًا حَكِيْمًا ﴿١٩﴾

19. Na ngawira (nyara) nyingi watakazozichukua, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.

وَعَدَكُمُ اللّٰهُ مَغَانِمَ كَثِيْرَةً تَاْخُذُوْنَهَا فَعَجَّلَ لَكُمْ هٰذِهٖ وَكَفَّ اَيْدِيَ النَّاسِ عَنْكُمْ وَلِتَكُوْنَ اٰيَةً لِّلْمُؤْمِنِيْنَ وَيَهْدِيَكُمْ صِرَاطًا مُّسْتَقِيْمًا ﴿٢٠﴾

20. Mwenyezi Mungu anakuahidini ngawira (nyara) nyingi mtakazozichukua; kisha amekuleteeni haya kwanza (kabla ya hayo); na akaizuia mikono ya watu isikufikieni, na ili iwe dalili (ya kheri) kwa Waislamu na kukuongozeni njia iliyonyoka.

وَّاُخْرٰى لَمْ تَقْدِرُوْا عَلَيْهَا ۗ قَدْ اَحَاطَ اللّٰهُ بِهَا ۗ وَكَانَ اللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرًا ﴿٢١﴾

21. Na (atakupeni ngawira) nyingine, hamjaweza kuzipata bado, (ambazo) Mwenyezi Mungu amekwishazizingia, na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

وَلَوْ قٰتَلَكُمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَوَلَّوُا الْاَدْبَارَ ثُمَّ لَا يَجِدُوْنَ وَلِيًّا وَّلَا نَصِيْرًا ﴿٢٢﴾

22. Na lau kama makafiri wangalipigana nanyi, bila shaka wangegeuza migongo (wakakimbia); kisha wasingalipata mlinzi wala msaidizi.

سُنَّةَ اللّٰهِ الَّتِيْ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلُ ۚ وَلَنْ تَجِدَ لِسُنَّةِ اللّٰهِ تَبْدِيْلًا ﴿٢٣﴾

23. Hiyo ndiyo kawaida ya Mwenyezi Mungu iliyotangulia zamani; wala hutapata mabadiliko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu.

وَهُوَ الَّذِيْ كَفَّ اَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَاَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ مِنْۢ بَعْدِ اَنْ اَظْفَرَكُمْ عَلَيْهِمْ ۗ وَكَانَ اللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرًا ﴿٢٤﴾

24. Na Yeye ndiye aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya kukupeni (Mwenyezi Mungu) ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu anaona (yote) mnayoyatenda.

هُمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَالْهَدْيَ مَعْكُوْفًا اَنْ يَّبْلُغَ مَحِلَّهٗ ۗ وَلَوْلَا رِجَالٌ مُّؤْمِنُوْنَ وَنِسَآءٌ مُّؤْمِنٰتٌ لَّمْ تَعْلَمُوْهُمْ اَنْ تَطَـُٔوْهُمْ فَتُصِيْبَكُمْ مِّنْهُمْ مَّعَرَّةٌۢ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۚ لِيُدْخِلَ اللّٰهُ فِيْ رَحْمَتِهٖ مَنْ يَّشَآءُ ۚ لَوْ تَزَيَّلُوْا لَعَذَّبْنَا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْهُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿٢٥﴾

25. Hao ndio waliokufuru na wakakuzuilieni kwenda katika Msikiti Mtukufu (wa Makaa baada ya kukaribia hapo kwa kiasi cha meli 48), na wakawazuilia wale wanyama (mliowachukua kwa ajili ya kuchinjwa) wasifike mahala pake. Na lau kama si wanaume Waislamu na wanawake Waislamu (walioko Makka wanaficha Uislamu wao), msiowafahamu, msije mkawasaga bila kujua, na kwa hiyo mkapate masikitiko kwa ajili yao; (ingalikuwa si haya Mungu asingekuzuieni kupigana nao. Amefanya haya) ili Mwenyezi Mungu amuingize amtakaye katika rehema yake. Kama (Waislamu na makafiri) wangalitengana, bila shaka tungaliwaadhibu wale waliokufuru miongoni mwao adhabu iumizayo.

---

22. Anawapa nguvu Mwenyezi Mungu hao Waislamu wa kweli. Na sisi tukiwa Waislamu wa kweli tutalipwa kama hivi:

Jaza Mola utujazi
Utuonye penye enzi
Nyoyo zitwishe simanzi
Ya Muinu Awnaka

Utupe kheri haraka
Utwepushie mashaka
Utupe tunayotaka
Iwe *Kun Fayakunu*

Hali zetu ni dhalili
Ndiwe wa kutujamili
Kwako twaomba fadhili
Amina Rabi Amina

Twakuombawe Rabana
Wala mwengine hatuna
Enzi yako Maulana
Iwe *Kun Fayakunu*

إِذْ جَعَلَ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْحَمِيَّةَ حَمِيَّةَ الْجَاهِلِيَّةِ فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ التَّقْوَىٰ وَكَانُوا أَحَقَّ بِهَا وَأَهْلَهَا ۚ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٢٦﴾

26. Pale wale waliokufuru walipotia nyoyoni mwao mori, mori wa ujinga; basi hapo Mwenyezi Mungu aliteremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya Waislamu; na akawalazimisha neno la kucha Mungu; nao walikuwa ndio wenye haki zaidi nalo na waliostahili. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

لَقَدْ صَدَقَ اللَّهُ رَسُولَهُ الرُّؤْيَا بِالْحَقِّ ۖ لَتَدْخُلُنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ آمِنِينَ مُحَلِّقِينَ رُءُوسَكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا تَخَافُونَ ۖ فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا فَجَعَلَ مِنْ دُونِ ذَٰلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿٢٧﴾

27. Kwa yakini Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ndoto yake ya haki: Bila shaka nyinyi mtaingia katika Msikiti Mtukufu Insha-Allah kwa salama; mkinyoa vichwa vyenu na mkipunguza nywele (kama ilivyo wajibu kufanya hivyo wakati wa Hija). Hamtakuwa na hofu (wakati huo). Na (Mwenyezi Mungu) anajua msiyoyajua. Basi kabla ya haya atakupeni kushinda (kwanza) kuliko karibu (kuwashinda Mayahudi).

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ ۚ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

28. Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi.

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ ۚ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ تَرَاهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا ۖ سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثَرِ السُّجُودِ ۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التَّوْرَاةِ ۚ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْأَهُ فَآزَرَهُ فَاسْتَغْلَظَ فَاسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِ يُعْجِبُ الزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ ۗ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾

29. Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu (pamoja), wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi (yake). Alama zao zi katika nyuso zao, kwa taathira, (athari) ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili (umetajwa hivi): Kuwa (wao) ni kama mmea uliotoa matawi yake; kisha (matawi hayo) yakautia nguvu; ukawa mnene ukasimama sawasawa juu ya kigogo chake, ukawafurahisha walioupanda; ili awakasirishe makafiri kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu amewaahidi walioamini na kutenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa.

---


27. Makadiyani mwisho wa maelezo ya Aya hii waliyoifanya ya 28 wametia ukafiri huu:- "Manabii ni wanaadamu tu, na pengine wanaweza kukosea kufahamu muradi hasa katika bishara za Mwenyezi Mungu, kama vile Mtume s.a.w. alivyokosea kufahamu muradi khasa katika ndoto yake." Ukafiri mkubwa kabisa huu: kuwa Mitume hufanya mambo, na hali ya kuwa sivyo walivyotakiwa kufanya, sivyo walivyoambiwa! Mtume hatamki kinyume na aliloambiwa, atafanya kinyume cha aliloambiwa? Mwenyezi Mungu anasema katika Aya ya 3 na ya 4 ya Surat *Wannajim:* "Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake) Hayakuwa haya (anayosema) ila ni Wahyi (ufunuo) uliofunuliwa kwake." Wao wanasema anafanya Mtume kinyume cha alivyoambiwa! Sababu ya kutia haya ni kumpigania huyo mtu wao. Yeye alijipa Utume na kujibandikiza kuletewa Wahyi, katika maneno yake na vitendo vyake. Na natija ya chungu ya vitendo vyake hivyo na maneno hayo ilikuwa mbaya kabisa kwake. Ndiyo maana wanamtafutia vipengee hapa kwa kusema kuwa Mitume wakati mwingine hufahamu vibaya Wahyi wa Mwenyezi Mungu, wakafanya ya kuwadhuru. Hastahiki kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu anayefahamu kinyume cha anavyoambiwa. Bali hafai hata kuwa mtumishi wa kufagia choo, anayefahamu kinyume cha anavyoambiwa; atastahiki kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Basi wameibanisha hapa daraja ya mjumbe wao.

Aliota Mtume katika mwaka wa 6 wa *Al Hijra* kuwa anahiji yeye na watu wake. Ndipo alipotoka akenda huko

Makka na Masahaba kiasi cha 1500. Wakazuiliwa na Maqureshi, kama tulivyobainisha katika Maelezo ya Aya ya 1 ya Sura hii hii. Basi Mwenyezi Mungu ndiyo anamwambia hapa kuwa atakwenda tu kuhiji na watu wake, salama usalmini, kwa hija iliyo kamili. Basi akahiji nao mwaka wa kumi wa *Al Hijra* na hali ya kuwa wanakaribia kuwa watu laki, badala ya wale alfu moja na mia tano.

28. Hii ni bishara ya kuwa Uislamu maisha utakuwa unatangaa — unakwenda mbele tu, kama tunavyoona.

29. Hapa wanatajwa Waislamu wazuri na namna walivyosifiwa katika Taurati na namna walivyosifiwa katika Injili. Basi natuwe hivi, ili tuwe Waislamu kweli, na tupate maghufira na huo ujira mwema.



Ina Aya 18

SURATUL HUJURAT
(Imeteremka Madina)

Ina Makara 2

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُقَدِّمُوْا بَيْنَ يَدَيِ اللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ۭ اِنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ①

1. Enyi mlioamini! Msitangulize (kusema lenu) mbele ya (neno la) Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na Mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَرْفَعُوْٓا اَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوْا لَهٗ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ اَنْ تَحْبَطَ اَعْمَالُكُمْ وَاَنْتُمْ لَا تَشْعُرُوْنَ ②

2. Enyi mlioamini! Msipaze sauti zenu kuliko sauti ya Mtume wala msiseme naye kwa sauti ya nguvu kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikakosa thawabu, na hali hamtambui.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَغُضُّوْنَ اَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُوْلِ اللّٰهِ اُولٰۗىِٕكَ الَّذِيْنَ امْتَحَنَ اللّٰهُ قُلُوْبَهُمْ لِلتَّقْوٰى ۭ لَهُمْ مَّغْفِرَةٌ وَّاَجْرٌ عَظِيْمٌ ③

3. Kwa hakika wale wanaoangusha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa kumuogopa Mungu. Basi yatakuwa kwao maghufira na thawabu kubwa (kabisa).

اِنَّ الَّذِيْنَ يُنَادُوْنَكَ مِنْ وَّرَاۗءِ الْحُجُرٰتِ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُوْنَ ④

4. Wale wanaokwita nyuma ya vyumba; (uko ndani kwako, wanakuja kukugongea madirisha na kukwita); wengi wao hawafahamu (adabu).

وَلَوْ اَنَّهُمْ صَبَرُوْا حَتّٰى تَخْرُجَ اِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ ۭ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ⑤

5. Na kama wangalingoja mpaka uwatokee, ingekuwa bora kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghufira (na) Mwenye rehema.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنْ جَاۗءَكُمْ فَاسِقٌۢ بِنَبَاٍ فَتَبَيَّنُوْٓا اَنْ تُصِيْبُوْا قَوْمًۢا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوْا عَلٰي مَا فَعَلْتُمْ نٰدِمِيْنَ ⑥

6. Enyi mlioamini! Kama fasiki, (asiyekuwa wa kutegemewa) akikujieni na habari (yoyote ile msimkubalie tu) bali pelelezeni (kwanza), msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda.

---

1. Haya ndiyo tunayoambiwa kila siku: kuwa maadamu iko kauli ya Mwenyezi Mungu na Mtume, basi isifuatwe kauli ya mwingine — itupiliwe mbali, kama alivyosema Imamu Shafii na wengine.

2-5. Baadhi ya mambo wanayokatazwa kumfanyia Mtume; bali na kila mkubwa anastahiki afanyiwe hishima.

6. Katika makatazo mazuri kabisa haya ya kutosikiliza maneno mabaya anayotajiwa nayo mtu nyuma yake, kwani mara nyingine — yanakuwa ya uwongo. Na yote haya ni kwa kuogopa yasitokee haya yaliyotajwa hapa na mengineyo.

وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ فِيْكُمْ رَسُوْلَ اللّٰهِ ۭ لَوْ يُطِيْعُكُمْ فِيْ
كَثِيْرٍ مِّنَ الْاَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ حَبَّبَ
اِلَيْكُمُ الْاِيْمَانَ وَزَيَّنَهٗ فِيْ قُلُوْبِكُمْ وَكَرَّهَ
اِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوْقَ وَالْعِصْيَانَ ۭ اُولٰۗىِٕكَ هُمُ
الرّٰشِدُوْنَ ۙ﴿۷﴾

7. Na jueni ya kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na nyiye. (Basi msikilizeni yeye anavyokuambieni). Lau yeye angekutiini katika mambo mengi (mnayoyasema) bila shaka mngetaabika. Lakini Mwenyezi Mungu ameupendezesha kwenu Uislamu na ameupamba nyoyoni mwenu, na amekufanyeni mchukie ukafiri na ufasiki na uasi. Hao ndio walioongoka

فَضْلًا مِّنَ اللّٰهِ وَنِعْمَةً ۭ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ
حَكِيْمٌ ﴿۸﴾

8. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na neema (zake mmepata haya). Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima.

وَاِنْ طَاۗىِٕفَتٰنِ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ اقْتَتَلُوْا فَاَصْلِحُوْا
بَيْنَهُمَا ۚ فَاِنْۢ بَغَتْ اِحْدٰىهُمَا عَلَي الْاُخْرٰى
فَقَاتِلُوا الَّتِيْ تَبْغِيْ حَتّٰى تَفِيْۗءَ اِلٰٓى اَمْرِ اللّٰهِ ۚ
فَاِنْ فَاۗءَتْ فَاَصْلِحُوْا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ
وَاَقْسِطُوْا ۭ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِيْنَ ﴿۹﴾

9. Na ikiwa makundi mawili katika Waislamu yanapigana, basi fanyeni suluhu baina yao; na likiwa moja la hayo linamdhulumu mwenziwe, basi lipigeni lile linaloonea mpaka lirudie katika amri ya Mwenyezi Mungu. Na kama likirudi, basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaohukumu kwa haki.

اِنَّمَا الْمُؤْمِنُوْنَ اِخْوَةٌ فَاَصْلِحُوْا بَيْنَ اَخَوَيْكُمْ ۚ
وَاتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ﴿۱۰﴾

10. Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na Mcheni Mwenyezi Mungu, (msipuuze jambo la kupatanisha) ili mrehemewe.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّنْ قَوْمٍ
عَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنُوْا خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَاۗءٌ
مِّنْ نِّسَاۗءٍ عَسٰٓى اَنْ يَّكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ ۚ

11. Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao; hwenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; hwenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitukanane

---

8. Tunaambiwa tuishukuru fadhila adhimu hii — neema kubwa hii ya kuwafikiwa Uislamu. *Alhamdu Lillah*

Al Hamdu Lillahi	Namshukuru Ilahi
Kunipa Dini Sahihi	Na kwa kunipa akili
Na vile kuniwezesha	Mengi nikabainisha
Bila ya kubabaisha	Haki ikawa batili.
Vingi nilivyovitunga	Nikazifichua kunga
"Yaso ndiyo" nikapinga	"Ya ndiyo" nikakubali.
Basi ninakushukuru	Mola Rahimu Ghafuru
Unizidishie nuru	Kiza kinondoke mbali.
Rabi yangu matulubu	Kutunga kusoharibu
Si Nukuta si Irabu	Yote yawe ni ya kweli.
Na hao ninowambiya	Wayafwate yote piya
Na yote yawe ya njia	Ya dini yako Jalili.
Tafsiri ya Qurani	Inatoka uwanjani
Iongoze ikhwani	Kwa zako nyingi fadhili.

9, 10. Wanahimizwa Waislamu hapa kweli kweli kupatanisha Waislamu wakigombana, hata baina ya mtu na mtu tu, seuze baina ya watu na watu. Na jambo hili lina thawabu kubwa kabisa, kama ilivyo katika Aya ya 114 ya *Suratun Nisaa* na nyinginezo. Na lina dhambi kubwa likipuuzwa — nao ni kukoseshwa rehema — kama ilivyo hapa na penginepo.

11. Makatazo makali kabisa juu ya kudharauliana, (kuzarauliana) na kuchekana na kubezana na kuambiwa

وَلَا تَلْمِزُوْٓا اَنْفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوْا بِالْاَلْقَابِ ؕ
بِئْسَ الِاسْمُ الْفُسُوْقُ بَعْدَ الْاِيْمَانِ ۚ وَمَنْ
لَّمْ يَتُبْ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ⑪

kwa kabila, wala msiitane kwa majina mabaya (ya kejeli): Jina baya kabisa kuambiwa mtu ni asi baada ya kuwa ni Muisilamu. (Na kufanya haya ni uasi) Na wasiotubu, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao).

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اجْتَنِبُوْا كَثِيْرًا مِّنَ
الظَّنِّ ۫ اِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ اِثْمٌ وَّلَا تَجَسَّسُوْا
وَلَا يَغْتَبْ بَّعْضُكُمْ بَعْضًا ؕ اَيُحِبُّ اَحَدُكُمْ اَنْ
يَّاْكُلَ لَحْمَ اَخِيْهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوْهُ ؕ
وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ تَوَّابٌ رَّحِيْمٌ ⑫

12. Enyi mlioamini! Jiepusheni sana na (kuwadhania watu) dhana (mbaya) kwani (kuwadhani watu) dhana (mbaya) ni dhambi. Wala msipeleleze (habari za watu). Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine. Je! Mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, Hampendi; (Basi na haya msiyapende). Na Mcheni Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba (na) Mwingi wa kurehemu.

يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ اِنَّا خَلَقْنٰكُمْ مِّنْ ذَكَرٍ وَّاُنْثٰى
وَجَعَلْنٰكُمْ شُعُوْبًا وَّقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوْا ؕ اِنَّ
اَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللّٰهِ اَتْقٰىكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌ
خَبِيْرٌ ⑬

13. Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja; Adamu) na (yule yule) mwanamke (mmoja; Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi; siyo mkejeleane). Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote).

قَالَتِ الْاَعْرَابُ اٰمَنَّا ؕ قُلْ لَّمْ تُؤْمِنُوْا
وَلٰكِنْ قُوْلُوْٓا اَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ الْاِيْمَانُ
فِيْ قُلُوْبِكُمْ ؕ وَاِنْ تُطِيْعُوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ لَا
يَلِتْكُمْ مِّنْ اَعْمَالِكُمْ شَيْـًٔا ؕ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ
رَّحِيْمٌ ⑭

14. Walisema wanaokaa jangwani (kumwambia Mtume): "Tumeamini." Sema (uwaambie) "Hamjaamini (kweli kweli bado), lakini semeni; Tumesilimu (Tumenyenyekea); maana imani haijaingia vyema nyoyoni mwenu bado. Na mkimtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hatakupunguzieni chochote katika (thawabu za) vitendo vyenu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

اِنَّمَا الْمُؤْمِنُوْنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ ثُمَّ
لَمْ يَرْتَابُوْا وَجٰهَدُوْا بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ فِيْ
سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ اُولٰٓئِكَ هُمُ الصّٰدِقُوْنَ ⑮

15. Wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; kisha wakawa si wenye shaka, na wakaipigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wenye kuamini kweli.

قُلْ اَتُعَلِّمُوْنَ اللّٰهَ بِدِيْنِكُمْ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ مَا
فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ؕ وَاللّٰهُ بِكُلِّ
شَيْءٍ عَلِيْمٌ ⑯

16. Sema: "Oh! Mnamjulisha Mwenyezi Mungu dini yenu (kwa uwongo)! Na hali Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na ardhini; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."

---

kuwa binadamu wote sawa sawa. Wote — weupe, wekundu, manjano na weusi — wamezaliwa na huyo huyo baba mmoja. Nabii Adamu na mama mmoja, Bibi Hawwa. Utukufu uko katika kumcha Mungu. Amchaye vilivyo zaidi ndiye bora zaidi. Na huyo (a) amchaye zaidi na (b) amchaye wastani na (c) amchaye kidogo; hawatambulikani hapa. Hata wenyewe hawajijui. Anaowajua ni Mwenyewe Subhana na atawadhihirisha hiyo siku ya Kiama.

14. Kuna watu wengi huwa wanafanya zile arkanul Islam zote — bila ya kuwa na Imani sawa sawa — basi ndio wanaotajwa hapa.


15. Hapa wanatajwa Waislamu wa kweli kweli. Basi natuwe watu hawa.

17. Wanakusumbulia kwa kuingia kwao Uislamuni. Sema, "Msifanye kuwa ni ihsani kwangu kusilimu kwenu, bali Mwenyezi Mungu ndiye aliyekufanyieni ihsani kwa kukuongozeni katika Uislamu, ikiwa nyinyi ni wakweli."

18. Bila shaka Mwenyezi Mungu anajua yaliyofichikana mbinguni na ardhini; na Mwenyezi Mungu anaona mnayoyatenda (yote).

يَمُنُّونَ عَلَيْكَ أَنْ أَسْلَمُوا ۖ قُلْ لَا تَمُنُّوا
عَلَيَّ إِسْلَامَكُمْ ۖ بَلِ اللَّهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ أَنْ
هَدَاكُمْ لِلْإِيمَانِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٧﴾
إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ غَيْبَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ
وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٨﴾

17. Kuna Waarabu wengine waliosilimu bila ya vita, basi wakamsumbulia Mtume kuwa wamesilimu bila ya yeye wala Waislamu wengine. Basi wanaambiwa, wao ndio wanaostahiki kusimuliwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwa amewawafikia Uislamu bila misukosuko, sio wao kuwasimulia watu.



Ina Aya 45 **SURAT QAF** *Ina Makara 3*

(Imeteremka Makka)

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

قٓ ۟ وَالْقُرْاٰنِ الْمَجِيْدِ ۝١

1. Qaf. Naapa kwa (hii) Qurani tukufu (kuwa mtafufuliwa).

بَلْ عَجِبُوْٓا اَنْ جَآءَهُمْ مُّنْذِرٌ مِّنْهُمْ فَقَالَ الْكٰفِرُوْنَ هٰذَا شَيْءٌ عَجِيْبٌ ۝٢

2. Bali wanastaajabu ya kwamba amewajia Muonyaji kutoka miongoni mwao (Wanataka awe Malaika). Na wakasema makafiri: "Hili ni jambo la ajabu!"

ءَاِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا ۚ ذٰلِكَ رَجْعٌۢ بَعِيْدٌ ۝٣

3. "Kuwa tutakapokufa na tukawa udongo (kuwa tutafufuliwa)? Marejeo hayo ni ya mbali kabisa; (hayawezi kuwa)."

قَدْ عَلِمْنَا مَا تَنْقُصُ الْاَرْضُ مِنْهُمْ ۚ وَعِنْدَنَا كِتٰبٌ حَفِيْظٌ ۝٤

4. Kwa hakika tunajua kiasi cha kila kinachopunguzwa na ardhi katika miili yao (wakati wanapooza huko makaburini). Na kwetu kiko Kitabu kinachohifadhi (kila kitu).

بَلْ كَذَّبُوْا بِالْحَقِّ لَمَّا جَآءَهُمْ فَهُمْ فِيْٓ اَمْرٍ مَّرِيْجٍ ۝٥

5. Lakini walikadhibisha haki ilipowajia. Na wamo katika jambo la mkorogeko.

اَفَلَمْ يَنْظُرُوْٓا اِلَى السَّمَآءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنٰهَا وَزَيَّنّٰهَا وَمَا لَهَا مِنْ فُرُوْجٍ ۝٦

6. Je! Hawazioni mbingu zilizo juu yao! Tumezijengaje na tumezipambaje. Wala hazina nyufa!

وَالْاَرْضَ مَدَدْنٰهَا وَاَلْقَيْنَا فِيْهَا رَوَاسِيَ وَاَنْۢبَتْنَا فِيْهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍۢ بَهِيْجٍ ۝٧

7. Na ardhi tumeitandaza na tukaiwekea milima, na tukaiotesha mimea mizuri ya kila namna.

تَبْصِرَةً وَّذِكْرٰى لِكُلِّ عَبْدٍ مُّنِيْبٍ ۝٨

8. (Yawe haya) ni kifumbua macho na ukumbusho kwa kila mtu muelekevu.

وَنَزَّلْنَا مِنَ السَّمَآءِ مَآءً مُّبٰرَكًا فَاَنْۢبَتْنَا بِهٖ جَنّٰتٍ وَّحَبَّ الْحَصِيْدِ ۝٩

9. Na tumeyateremsha kutoka mawinguni maji yaliyobarikiwa, na kwa hayo tukaotesha mabustani na nafaka zivunwazo.

وَالنَّخْلَ بٰسِقٰتٍ لَّهَا طَلْعٌ نَّضِيْدٌ ۝١٠

10. Na mitende mirefu yenye makole yaliyozaa kochokocho

رِّزْقًا لِّلْعِبَادِ ۙ وَاَحْيَيْنَا بِهٖ بَلْدَةً مَّيْتًا ۭ كَذٰلِكَ الْخُرُوْجُ ۝١١

11. Kiwe chakula kwa ajili ya waja (wangu). Na tukaufufua kwa hiyo (mvua) mji uliokufa; Basi namna hivi ndivyo utakavyokuwa ufufuaji.

---

1. Hii ni Sura ambayo Mtume akiisoma sana katika Hafla kubwa na Sala kubwa, kama Sala za Idi na Ijumaa, kwa ajili ya mawaidha yake makubwa yaliyomo humo.

4-16. Unatajwa Ujuzi wa Mwenyezi Mungu na Uweza wake.

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَّأَصْحٰبُ الرَّسِّ وَثَمُودُ ﴿١٢﴾

12. Walikadhibisha kabla yao watu wa Nuhu na wakazi wa Rass na Thamudi

وَعَادٌ وَّفِرْعَوْنُ وَإِخْوَانُ لُوطٍ ﴿١٣﴾

13. Na Adi na Firauni na watu wa Luti

وَّأَصْحٰبُ الْأَيْكَةِ وَقَوْمُ تُبَّعٍ ۚ كُلٌّ كَذَّبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ وَعِيدِ ﴿١٤﴾

14. Na wakazi wa kichakani, (Watu wa Nabii Shuebu) na watu wa Tubba (Yaman). Wote waliwakadhibisha Mitume; kwa hivyo onyo langu likathubutika (juu yao).

أَفَعَيِينَا بِالْخَلْقِ الْأَوَّلِ ۚ بَلْ هُمْ فِي لَبْسٍ مِّنْ خَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٥﴾

15. Je! Tulichoka kwa kuumba kwa mara ya kwanza (hata tushindwe kuumba kwa umbo la pili)? Basi wao wamo katika shaka tu juu ya umbo jipya!

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ وَنَعْلَمُ مَا تُوَسْوِسُ بِهِ نَفْسُهُ ۖ وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ ﴿١٦﴾

16. Na bila shaka tumemuumba mtu; nasi tunajua yanayopita katika nafsi yake; nasi tukaribu naye zaidi kuliko mshipa wa shingo (yake).

إِذْ يَتَلَقَّى الْمُتَلَقِّيَانِ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ قَعِيدٌ ﴿١٧﴾

17. Wanapopokea wapokeaji wawili, anayekaa kuli[illegible]anayekaa) kushotoni, (Malaika).

مَا يَلْفِظُ مِن قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٨﴾

18. Hatoi kauli yoyote isipokuwa karibu naye yuko mngojeaji tayari (kuandika).

وَجَاءَتْ سَكْرَةُ الْمَوْتِ بِالْحَقِّ ۖ ذٰلِكَ مَا كُنتَ مِنْهُ تَحِيدُ ﴿١٩﴾

19. Na kutoka roho kutakapomjia kwa haki. (Hapo ataambiwa): "Hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia."

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ ۚ ذٰلِكَ يَوْمُ الْوَعِيدِ ﴿٢٠﴾

20. Na itapulizwa parapanda (Baragumu); hiyo ndiyo Siku ya makamio, (siku ya Kiama).

وَجَاءَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّعَهَا سَائِقٌ وَشَهِيدٌ ﴿٢١﴾

21. Na itakuja kila nafsi pamoja na mchungaji (wake) na shahidi (wake).

لَّقَدْ كُنتَ فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هٰذَا فَكَشَفْنَا عَنكَ غِطَاءَكَ فَبَصَرُكَ الْيَوْمَ حَدِيدٌ ﴿٢٢﴾

22. (Aambiwe): "Kwa hakika ulikuwa umo katika ghafla na jambo hili. Basi tumekuondolea (leo) pazia yako; kuona kwako leo kumekuwa kukali."

وَقَالَ قَرِينُهُ هٰذَا مَا لَدَيَّ عَتِيدٌ ﴿٢٣﴾

23. Na yule (Malaika) aliyekuwa pamoja naye (akiandika amali zake) atasema (kumwambia Malaika wa adhabu): "Hayo ndiyo yaliyowekwa tayari kwangu (ya amali zake mbovu hizi)."

أَلْقِيَا فِي جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ عَنِيدٍ ﴿٢٤﴾

24. (Wakati huo kutasemwa): "Mtupeni katika Jahanamu kila kafiri asi,"

مَّنَّاعٍ لِّلْخَيْرِ مُعْتَدٍ مُّرِيبٍ ﴿٢٥﴾

25. "Akatazaye kheri, arukaye mipaka, aliyekuwa akijipa shaka (zisizokuwa na sababu)

الَّذِي جَعَلَ مَعَ اللَّهِ إِلٰهًا آخَرَ فَأَلْقِيَاهُ فِي الْعَذَابِ

26. Aliyeweka mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, basi mtupeni katika adhabu kali

17-35. Inabainishwa namna Malaika wanavyodhibiti maneno na vitendo vya watu wema na wabaya na namna watakavyolipwa.

(pamoja na huyo mwenziwe waliokuwa wakipotezana).”

الشَّدِيدِ ﴿٢٧﴾

27. Mwenzake aseme: “Ee Mola wetu! Sikumpoteza mimi, bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotofu (upotevu) wa mbali kabisa (na haki).”

قَالَ قَرِينُهُ رَبَّنَا مَا أَطْغَيْتُهُ وَلَٰكِن كَانَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿٢٧﴾

28. Aseme (Mwenyezi Mungu): “Msigombane mbele yangu, Nilikwisha kukutangulizeni onyo (langu).”

قَالَ لَا تَخْتَصِمُوا لَدَيَّ وَقَدْ قَدَّمْتُ إِلَيْكُم بِالْوَعِيدِ ﴿٢٨﴾

29. “Kauli yangu haibadilishwi kwangu, wala Mimi Siwadhulumu waja wangu.”

مَا يُبَدَّلُ الْقَوْلُ لَدَيَّ وَمَا أَنَا بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٢٩﴾

30. Siku tutakayoiambia Jahanamu: “Je! Umejaa?” Nayo itasema: “Je! Kuna zaidi (zaidi? Naije tu!).”

يَوْمَ نَقُولُ لِجَهَنَّمَ هَلِ امْتَلَأْتِ وَتَقُولُ هَل مِن مَّزِيدٍ ﴿٣٠﴾

31. Na Pepo italetwa karibu, kwa wamchao Mungu, haitakuwa mbali (nao).

وَأُزْلِفَتِ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِينَ غَيْرَ بَعِيدٍ ﴿٣١﴾

32. Haya ndiyo mnayoahidiwa, kwa kila aelekeaye (kwa Mwenyezi Mungu), ajilindaye (na maasia).

هَٰذَا مَا تُوعَدُونَ لِكُلِّ أَوَّابٍ حَفِيظٍ ﴿٣٢﴾

33. Na anayemuogopa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa kurehemu, na hali ya kuwa hamuoni, na akaja kwa moyo ulioelekea (kwa Mwenyezi Mungu)

مَّنْ خَشِيَ الرَّحْمَٰنَ بِالْغَيْبِ وَجَاءَ بِقَلْبٍ مُّنِيبٍ ﴿٣٣﴾

34. (Waambiwe): “Ingieni (Pepo) kwa salama.” Hiyo ni siku ya kukaa daima (katika starehe za huko Peponi).

ادْخُلُوهَا بِسَلَامٍ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْخُلُودِ ﴿٣٤﴾

35. Humo watapata chochote wakitakacho; na Kwetu kuna zaidi (ya kila wakitakacho).

لَهُم مَّا يَشَاءُونَ فِيهَا وَلَدَيْنَا مَزِيدٌ ﴿٣٥﴾

36. Na uma ngapi tumeziangamiza kabla yao; waliokuwa na nguvu zaidi kuliko wao. Nao walitembea katika nchi nyingi, lakini je yako makimbilio? (Waliangamizwa tu na Mwenyezi Mungu).

وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُم مِّن قَرْنٍ هُمْ أَشَدُّ مِنْهُم بَطْشًا فَنَقَّبُوا فِي الْبِلَادِ هَلْ مِن مَّحِيصٍ ﴿٣٦﴾

37. Kwa yakini katika jambo hili mna ukumbusho kwa mwenye moyo au kwa ategaye sikio, naye mwenyewe awe hadhiri.

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَذِكْرَىٰ لِمَن كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ ﴿٣٧﴾

38. Na tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao katika nyakati sita, wala hayakutugusa machofu.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا مَسَّنَا مِن لُّغُوبٍ ﴿٣٨﴾

39. Basi vumilia kwa hayo wasemayo, na Mtukuze Mola wako kwa kumsifu, kabla ya kutoka jua, (sala ya Asubuhi) na kabla ya kuchwa, (Adhuhuri na Laasiri).

فَاصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ ﴿٣٩﴾

---

38. Tumetaja katika Aya ya 4 ya *Suratus Sajda* muradi wa hizi siku.

وَمِنَ الَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَأَدْبَارَ السُّجُودِ ﴿٤٠﴾

40. Na katika usiku pia Mtukuze. (Sala ya Magharibi na Isha); na pia baada ya kusujudu, (baada ya kusali Sala za Fardhi usali suna za Baadiya. Na kablia kabla ya kusali sala za Faradhi).

وَاسْتَمِعْ يَوْمَ يُنَادِ الْمُنَادِ مِن مَّكَانٍ قَرِيبٍ ﴿٤١﴾

41. Na sikia, (ukumbuke) Siku atakayonadi mnadi kutoka mahali pa karibu (yao)

يَوْمَ يَسْمَعُونَ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْخُرُوجِ ﴿٤٢﴾

42. Siku watakayosikia ukelele wa haki; hiyo ndiyo Siku ya kutoka (makaburini).

إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي وَنُمِيتُ وَإِلَيْنَا الْمَصِيرُ ﴿٤٣﴾

43. Bila shaka sisi tunahuisha na tunafisha, na marejeo ni Kwetu


يَوْمَ تَشَقَّقُ الْأَرْضُ عَنْهُمْ سِرَاعًا ذَٰلِكَ حَشْرٌ عَلَيْنَا يَسِيرٌ ﴿٤٤﴾

44. (Wakumbushe) Siku itakapowapasukia ardhi, (watoke) humo upesi upesi; huo ni mkusanyo rahisi kwetu.

نَّحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ وَمَا أَنتَ عَلَيْهِم بِجَبَّارٍ ۖ فَذَكِّرْ بِالْقُرْآنِ مَن يَخَافُ وَعِيدِ ﴿٤٥﴾

45. Sisi tunajua sana wanayoyasema. Wala wewe si mwenye kuwatawalia; Mkumbushe kwa Qurani anayeogopa onyo langu.

41-44. Yanatajwa baadhi ya yatakayotokea Kiama.



Ina Aya 60

SURATUDH DHAARIYAT
(Imeteremka Makka)

Ina Makara 3

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

وَالذّٰرِيٰتِ ذَرْوًا ۝١

1. Naapa kwa pepo zinazotawanya (mvua) barabara

فَالْحٰمِلٰتِ وِقْرًا ۝٢

2. Zinazobeba mizigo (ya mawingu)

فَالْجٰرِيٰتِ يُسْرًا ۝٣

3. Zikenda nayo (mawingu hayo) kwa upole

فَالْمُقَسِّمٰتِ اَمْرًا ۝٤

4. Kisha zikayagawanya (hayo mawingu) kwa amri (ya Mwenyezi Mungu. Kisha kila moja likanyeshe mahala pake)

اِنَّمَا تُوْعَدُوْنَ لَصَادِقٌ ۝٥

5. Bila shaka mnayoahidiwa ni kweli

وَّاِنَّ الدِّيْنَ لَوَاقِعٌ ۝٦

6. Na kwa hakika malipo bila shaka yatatokea.

وَالسَّمَآءِ ذَاتِ الْحُبُكِ ۝٧

7. Naapa kwa mbingu hizi zenye sura nzuri,

اِنَّكُمْ لَفِيْ قَوْلٍ مُّخْتَلِفٍ ۝٨

8. Kuwa nyinyi muko katika kauli inayohitilafiana (katika kuupinga Uislamu).

يُّؤْفَكُ عَنْهُ مَنْ اُفِكَ ۝٩

9. Anageuzwa na haki kwa kauli hiyo anayegeuzwa.

قُتِلَ الْخَرّٰصُوْنَ ۝١٠

10. Wazushi wameangamizwa

الَّذِيْنَ هُمْ فِيْ غَمْرَةٍ سَاهُوْنَ ۝١١

11. Ambao wamo katika ujinga; wanapumbazika (katika ujinga huo)

يَسْـَٔلُوْنَ اَيَّانَ يَوْمُ الدِّيْنِ ۝١٢

12. Wanauliza (kwa mchezo, wanasema): "Ni lini (kuja kwake hiyo) Siku ya Hukumu?"

يَوْمَ هُمْ عَلَى النَّارِ يُفْتَنُوْنَ ۝١٣

13. Hiyo Siku watakayoadhibiwa Motoni.

ذُوْقُوْا فِتْنَتَكُمْ هٰذَا الَّذِيْ كُنْتُمْ بِهٖ تَسْتَعْجِلُوْنَ ۝١٤

14. (Waambiwe): "Onjeni adhabu yenu! Haya ndiyo mliyokuwa mkiyahimiza."

اِنَّ الْمُتَّقِيْنَ فِيْ جَنّٰتٍ وَّعُيُوْنٍ ۝١٥

15. Kwa yakini wamchao Mwenyezi Mungu watakuwa katika Mabustani na chemchem.

اٰخِذِيْنَ مَآ اٰتٰىهُمْ رَبُّهُمْ ۭ اِنَّهُمْ كَانُوْا قَبْلَ ذٰلِكَ مُحْسِنِيْنَ ۝١٦

16. Wanapokea aliyowapa Mola wao. Kwa hakika wao walikuwa wakifanya wema kabla ya haya.

15-19. Jaza watakayolipwa watu wema, na wepi hao watu wema.

كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ الَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ ﴿١٧﴾

17. Walikuwa wakilala kidogo tu usiku.

وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿١٨﴾

18. Na wakiomba maghufira, (msamaha) nyakati za kabla ya alfajiri.

وَفِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿١٩﴾

19. Na katika mali zao ilikuwako haki ya kupewa masikini aombaye na ajizuiaye kuomba.

وَفِي الْأَرْضِ آيَاتٌ لِّلْمُوقِنِينَ ﴿٢٠﴾

20. Na katika ardhi zimo (alama namna kwa namna za kuonyesha kuwapo Mwenyezi Mungu) kwa wenye yakini

وَفِي أَنفُسِكُمْ ۚ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٢١﴾

21. Na katika nafsi zenu (pia zimo alama hizo). Je! Hamuoni?

وَفِي السَّمَاءِ رِزْقُكُمْ وَمَا تُوعَدُونَ ﴿٢٢﴾

22. Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyoahidiwa.

فَوَرَبِّ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِنَّهُ لَحَقٌّ مِّثْلَ مَا أَنَّكُمْ تَنطِقُونَ ﴿٢٣﴾

23. Basi naapa kwa Mola wa mbingu na ardhi, kuwa hakika haya ni haki, kama ilivyo (haki) ya kwamba nyinyi mnasema.

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ ضَيْفِ إِبْرَاهِيمَ الْمُكْرَمِينَ ﴿٢٤﴾

24. Je! Imekujia hadithi ya wageni wahishimiwao wa (Nabii) Ibrahimu?

إِذْ دَخَلُوا عَلَيْهِ فَقَالُوا سَلَامًا ۖ قَالَ سَلَامٌ ۖ قَوْمٌ مُّنكَرُونَ ﴿٢٥﴾

25. Walipoingia kwake wakasema: "Salaam (Alaykum);" na (yeye Ibrahimu) akasema: "(Alaykumus) Salaam." (Na katika moyo wake anasema): "Ninyi watu nisiokujueni."

فَرَاغَ إِلَىٰ أَهْلِهِ فَجَاءَ بِعِجْلٍ سَمِينٍ ﴿٢٦﴾

26. Mara akaenda kwa ahali yake na akaleta ndama aliyenona

فَقَرَّبَهُ إِلَيْهِمْ قَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٢٧﴾

27. Akampeleka karibu yao. (Walipokuwa hawajanyosha mikono kula) Alisema: "Mbona hamuli!"

فَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً ۖ قَالُوا لَا تَخَفْ ۖ وَبَشَّرُوهُ بِغُلَامٍ عَلِيمٍ ﴿٢٨﴾

28. Basi akawatilia shaka (katika nafsi yake; akawaogopa akaona labda maadui zake). Wakasema: "Usiogope," na wakamtolea habari nzuri za (kuwa atazaa) mtoto mwenye ilimu.

فَأَقْبَلَتِ امْرَأَتُهُ فِي صَرَّةٍ فَصَكَّتْ وَجْهَهَا وَقَالَتْ عَجُوزٌ عَقِيمٌ ﴿٢٩﴾

29. Ndipo mkewe (Nabii Ibrahimu) akawaelekea, na huku anasema na akijipiga usoni kwa mastaajabu na kusema: "Mwanamke mzee, tasa (nitazaa)."

قَالُوا كَذَٰلِكِ قَالَ رَبُّكِ ۖ إِنَّهُ هُوَ الْحَكِيمُ الْعَلِيمُ ﴿٣٠﴾

30. Wakasema: "Ndivyo vivyo hivyo (utazaa, na hali ya kuwa wewe ni tasa). Amesema Mola wako. Hakika Yeye ndiye Mwenye hikima, Ajuaye (kila kitu)."

24-27. Kisa cha wageni wa Nabii Ibrahimu na namna inavyopasa kuwapokea wageni: kwa uchangamshi na kuwatengenezea chakula upesi — japokuwa hawajui — na kuwashughulikia katika kula kwao.

29. Kuonyesha kuwa mwanamke— akiwa yumo katika mavazi yake kamili — anaweza kuwatokea wanaume na kusema nao maneno yaliyo laiki na hapo.

قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ أَيُّهَا الْمُرْسَلُونَ ﴿٣١﴾

31. Akasema, "Basi makusudio yenu (mengine) ni nini, Enyi mliotumwa?"

قَالُوا إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمٍ مُجْرِمِينَ ﴿٣٢﴾

32. Wakasema: "Hakika sisi tumetumwa Tukawaangamize wale watu waovu (watu wa Nabii Luti)."

لِنُرْسِلَ عَلَيْهِمْ حِجَارَةً مِنْ طِينٍ ﴿٣٣﴾

33. "Ili tuwatupie juu yao mawe ya udongo (wa Motoni)".

مُسَوَّمَةً عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُسْرِفِينَ ﴿٣٤﴾

34. "Yaliyotiwa alama kwa Mola wako kwa ajili ya hao watu wanaopindukia mipaka katika maasia."

فَأَخْرَجْنَا مَنْ كَانَ فِيهَا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٣٥﴾

35. (Mwenyezi Mungu anasema): "Kwa hivyo Tukawatoa wale walioamini waliokuwa humo (ili adhabu isiwafike)".

فَمَا وَجَدْنَا فِيهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٣٦﴾

36. Lakini Hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu.

وَتَرَكْنَا فِيهَا آيَةً لِلَّذِينَ يَخَافُونَ الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٣٧﴾

37. Na (baada ya kuwaangamiza) Tukaacha humo alama kwa ajili ya wale wanaoogopa adhabu iumizayo.

وَفِي مُوسَىٰ إِذْ أَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ بِسُلْطَانٍ مُبِينٍ ﴿٣٨﴾

38. Na katika (habari za) Musa (ziko alama vile vile), Tulipompeleka kwa Firauni na hoja wazi kabisa.

فَتَوَلَّىٰ بِرُكْنِهِ وَقَالَ سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ ﴿٣٩﴾

39. Lakini akakengeuka (asiyafuate hayo) kwa sababu ya nguvu zake na akasema: "Huyu ni mchawi au ni mwandawazimu".

فَأَخَذْنَاهُ وَجُنُودَهُ فَنَبَذْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ وَهُوَ مُلِيمٌ ﴿٤٠﴾

40. Basi Tukamkamata (tukamtia mkononi) yeye na majeshi yake na Tukawatupa baharini, na mwenyewe alikuwa mlaumiwa.

وَفِي عَادٍ إِذْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الرِّيحَ الْعَقِيمَ ﴿٤١﴾

41. Na katika (habari za), Adi (ziko alama kadhalika). (Kumbusha) Tulipowapelekea upepo wa papazi uangamizao.

مَا تَذَرُ مِنْ شَيْءٍ أَتَتْ عَلَيْهِ إِلَّا جَعَلَتْهُ كَالرَّمِيمِ ﴿٤٢﴾

42. Haukuacha chochote ulichokijia ila ulikifanya kama kamba mbovu.

وَفِي ثَمُودَ إِذْ قِيلَ لَهُمْ تَمَتَّعُوا حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٤٣﴾

43. Na katika (habari za) Thamudi (ziko alama vile vile), (Kumbusha) walipoambiwa: "Jifurahisheni kwa muda mdogo tu. (Sasa hivi itakuja adhabu ikuangamizeni)."

فَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ فَأَخَذَتْهُمُ الصَّاعِقَةُ وَهُمْ يَنْظُرُونَ ﴿٤٤﴾

44. Wakaasi (wakakataa kwa jeuri) amri ya Mola wao; mara moto wa Radi uliwatoa roho zao na huku wanaona.

31-37. Kunatajwa kuangamizwa kwa watu wa Nabii Luti.
38-46. Kunatajwa kuangamiya uma za Mitume wengine.